
East African Journal of Swahili Studies, Volume 3, Issue 1, 2021
Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.335




**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 3, Issue 1, 2021**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Maelezo Kinzani ya Vipengele vya Sarufi ya Kiswahili Katika Vitabu Teule vya Shule za Upili Nchini Kenya

*Wanyonyi Fred Wanjala[1], Dkt. Misiko David Wasike, PhD[1] na Dkt. Fred Wanjala Simiyu, PhD[1]*

[1] Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine, Chuo Kikuu cha Kibabii, S.L.P 1699 – 50200, Nairobi, Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: wsimiyu@kibu.ac.ke

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.335**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*01 Juni 2021*

**Istilahi Muhimu**:

*Sarufi, Sarufi Amilifu, Vipengele Tata, Ujifunzaji Kitajiriba, Nomino Za Kawaida, Nomino Za Mguso, Kizuiwa Kwamiza, Kirai.*

**IKISIRI**

Dhamira ya makala hii ilikuwa ni kuonesha tofauti za kimaelezo baina ya waandishi wa sarufi kama inavyojitokeza katika ufundishaji na ujifunzaji wa Sarufi ya Kiswahili katika shule za upili hapa nchini Kenya. Uchunguzi huu uliongozwa na Nadharia ya Sarufi Amilifu na nadharia ya Ujifunzaji Kitajiriba. Sarufi Amilifu ni ya Simon C. Dik (1978). Nadharia hii inashikilia kwamba, uzingatifu wa sarufi ya lugha unadhihirika katika utendaji wa lugha hiyo ambao unakuzwa katika matini inayoandaliwa na wataalamu wake. Nayo nadharia ya Ujifunzaji Kitajiriba iliyoasisiwa na David Allen Kolb mnamo mwaka wa 1984 inaangazia matumizi ya tajiriba katika ufundishaji na ujifunzaji. Kundi lengwa lilikuwa ni waandishi wa Sarufi ya Kiswahili, walimu wa Sarufi ya Kiswahili na wanafunzi wa kidato cha tatu. Tulitumia mbinu za usampulishaji wa kinasibu na usampulishaji wa kimakusudi kuteua sampuli iliyokusudiwa tukizingatia asilimia 30 ya jumla ya idadi lengwa. Walimu 12 na wanafunzi 120 waliteuliwa kushiriki katika uchunguzi huu. Data ilikusanywa kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi wa yaliyomo, hojaji na mahojiano. Data katika makala hii iliwasilishwa kupitia maelezo, majedwali na asilimia. Matokeo ya makala hii yalionesha kwamba, waandishi wa Sarufi ya Kiswahili wanakinzana katika ufafanuzi wa baadhi ya vipengele vya Sarufi ya Kiswahili katika shule za upili nchini Kenya.

Uchunguzi huu utakuwa wenye umuhimu kwa walimu wa Sarufi ya Kiswahili, wanafunzi, wataalamu wa Sarufi ya Kiswahili na wale wanaoandaa na kuchapisha vitabu vya Sarufi ya Kiswahili kwa kutambua vipengele tata katika Sarufi ya Kiswahili. Makala ilipendekeza Taasisi ya Ukuzaji wa Mitalaa ya Kenya kuvichunguza upya vitabu vya kiada na ziada vya Sarufi ya Kiswahili ambavyo vimeidhinishwa na wao huku vikiwa na tofauti za kimaelezo.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

**APA CITATION**

Wanjala, W. F., Wasike, M. D., & Simiyu, F. W. (2021). Maelezo Kinzani ya Vipengele vya Sarufi ya Kiswahili Katika Vitabu Teule vya Shule za Upili Nchini Kenya. *East African Journal of Swahili Studies*, *3*(1), 30-50. https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.335.

**CHICAGO CITATION**

Wanjala, Wanyonyi Fred., Wasike, Misiko David., and Simiyu, Fred Wanjala. 2021. "Maelezo Kinzani ya Vipengele vya Sarufi ya Kiswahili Katika Vitabu Teule vya Shule za Upili Nchini Kenya". *East African Journal of Swahili Studies* 3 (1), 30-50. https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.335.

**HARVARD CITATION**

Wanjala, W. F. Wasike, M. D., and Simiyu, F. W. (2021) "Maelezo Kinzani ya Vipengele vya Sarufi ya Kiswahili Katika Vitabu Teule vya Shule za Upili Nchini Kenya", *East African Journal of Swahili Studies*, 3(1), pp. 30-50. doi: 10.37284/eajss.3.1.335.

**IEEE CITATION**

W. F. Wanjala, M. D. Wasike, and F. W. Simiyu, "Maelezo Kinzani ya Vipengele vya Sarufi ya Kiswahili Katika Vitabu Teule vya Shule za Upili Nchini Kenya", *EAJSS*, vol. 3, no. 1, pp. 30-50, June. 2021.

**MLA CITATION**

Wanjala, Wanyonyi Fred., Wasike, Misiko David., and Simiyu, Fred Wanjala. "Maelezo Kinzani ya Vipengele vya Sarufi ya Kiswahili Katika Vitabu Teule vya Shule za Upili Nchini Kenya". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 3, no. 1, June. 2021, pp. 30-50, doi:10.37284/eajss.3.1.335.

## UTANGULIZI

Sarufi ya lugha ina maana tofauti kwa watu tofauti kulingana na wataalamu wa sarufi Navaz na Sama (2018) ambao walihoji kwamba, aghalabu ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi unajikita tu katika uzingatiaji wa sheria za lugha. Ufundishaji na ujifunzaji huu unategemea kwa kiasi kikubwa matini ya waandishi ambao wanafafanua dhana na vipengele mbalimbali katika lugha. Lugha ya Kiswahili haijawachwa nyuma katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi yake. Hapa nchini Kenya, Sarufi ya Kiswahili inafunzwa kama sehemu mojawapo ya somo la Kiswahili ambalo ni la lazima katika shule za upili nchini Kenya (Timammy na Oduor, 2016). Kama wanavyodai Navaz na Sama (2018) kwamba sarufi ina maana tofauti kwa watu tofauti, wataalamu wengi wa lugha wamejitosa ulingoni kufafanua maana ya sarufi. Wasomi O'Grady, Dobrovolsky na Katamba (1996) walidahili kwamba, sarufi ni sheria zinazodhibiti matumizi ya lugha ambazo hukuzwa katika hatua za mwanzo katika upataji wa lugha huku wazawa wa lugha husika wakizikuza zaidi katika umri wa utotoni. Nao wanaisimu Massamba, Kihore na Hokororo (1999) wanaiona sarufi kama nguzo ambayo inadhibiti matawi ya isimu ya lugha. Habibu (2017) na Bruno (2020) pia wanaichambua sarufi kama sheria zinazotoa mwelekeo katika matumizi ya lugha yoyote ile.

Wapo wasomi wengine wanaoiona sarufi kama somo wakiwemo Leigh (2007) aliyedokeza kuwa, sarufi ni somo ambalo linachambua sheria za lugha ambazo zinadhibiti matumizi ya lugha hiyo. Katika utafiti huu, tulichukulia sarufi kuwa sheria ambazo zinaongoza ufundishaji na ujifunzaji wa lugha huku tukilenga lugha ya Kiswahili. Katika uchambuzi wetu, tulichunguza tofauti za kimaelezo katika kazi za waandishi wa Sarufi ya Kiswahili. Dhamira yetu ilihusu kubainisha vipengele tata ambavyo vinasababisha mitazamo kinzani kwa kuleta changamoto katika ufundishaji na ujifunzaji wa Sarufi ya Kiswahili. Kuhusiana na dhana ya vipengele tata, tulivichukulia kuwa ni mada ambazo zina ufafanuzi unaokinzana kwa mujibu wa waandishi mbalimbali wa Sarufi ya Kiswahili.

Tofauti za kimaelezo katika suala lolote lile ni jambo ambalo linatokana na mitazamo tofauti miongoni mwa binadamu. Kulingana na Wong na Bar-Yam (2017), binadamu hutofautiana na mwenzake kisaikolojia na kiisimu. Tofauti hizi hutokana na mitazamo ya kibinafsi au tajiriba mbalimbali walizo nazo binadamu. Kolb na Kolb (2011) walielekeza kwamba, namna tajiriba ya mtu inavyokuzwa ndivyo anavyoibua matokeo mapya katika mazingira yake. Isimu ni uchunguzi wa lugha kisayansi ambapo wataalamu mbalimbali wamefanya utafiti kuihusu. Uchunguzi wa baadhi ya wataalamu umekuwa ukilenga kuvumbua maumbo ya maneno katika lugha na matumizi yake. Miongoni mwa wataalamu hawa ni waandishi wa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.335

Sarufi ya Kiswahili ambao wametafiti na kuandika kuhusu Sarufi ya Kiswahili. Tulikusudia kuchunguza matini ya waandishi hawa ili tubainishe tofauti zilizopo miongoni mwao na namna ambavyo tofauti hizi zinavyosababisha changamoto katika ufundishaji na ujifunzaji wa Sarufi ya Kiswahili. Ili kuzitambua changamoto hizi katika hali halisi, tuliutekeleza utafiti huu katika eneo la Kaunti Ndogo ya Kimilili, Bungoma, kwa nia ya kupata fasili, maoni, mielekeo na mitazamo ya walimu wa Sarufi ya Kiswahili na wanafunzi kuhusu tofauti za kimaelezo miongoni mwa waandishi wa Sarufi ya Kiswahili.

**Misingi ya Nadharia**

Makala hii iliongozwa na nadharia mbili. Ya kwanza ni Nadharia ya Sarufi Amilifu ya Simon C. Dik (1978) huku ya pili ikiwa ni Nadharia ya Ujifunzaji Kitajiriba ya David Allen Kolb (1984). Nadharia hii inahoji kwamba, sarufi amilifu ni matumizi ya lugha kiutendaji ambapo lugha hii inachunguzwa namna inavyotumika katika kufaulisha mawasiliano miongoni mwa binadamu. Katika uchambuzi wa Sarufi Amilifu, Dik (1978) alieleza kile alichokiita uamilifu halisi wa lugha. Alidokeza kwamba, uamilifu halisi wa lugha ni hatua ya kuzingatia kanuni za matumizi ya lugha ili kuwasilisha maana katika mawasiliano. Maana hii ndiyo nguzo ya mawasiliano kwa sababu kupitia mawasiliano ndipo utendaji wa lugha hudhihirika.

Nadharia ya Sarufi Amilifu imejengeka katika mihimili mitatu. Mhimili wa kwanza ni wa utambuzi wa uhusiano kati ya wanajamii. Hapa, nadharia hii inaangazia namna lugha inavyotumika katika jamii kwa ajili ya kukuza na kuhifadhi uhusiano baina ya wanajamii. Lugha kama mojawapo ya amali katika jamii, huhifadhi utamaduni, itikadi na mila za wanajamii.

Mhimili wa pili ni wa kiutambuzi ambapo lugha inatumika hususan kutambulisha mazingira wanamokaa binadamu. Katika utambuzi huu, binadamu anaelewa mazingira yake kwa kutumia lugha ambapo lugha inatumika katika kufahamisha jamii kuhusu masuala mbalimbali katika jamii kama vile elimu, siasa na uchumi.

Mhimili wa tatu ni wa kiumatini ambapo lugha inatumika kama nyenzo ya kufanikisha mawasiliano kupitia miktadha mbalimbali kama vile habari, maandishi, ishara na makala anuwai. Mhimili huu unajikita katika matumizi ya lugha kwa kuzingatia sheria za lugha almaarufu sarufi ili kuepuka kuvuruga mawasiliano. Aidha, kuibuka kwa matini yaliyo sanifu hukuza lugha kiutendaji. Kuhusiana na hili, Dik (1978) anaiona matini kama kifaa kizuri cha kuonesha namna uamilifu wa sarufi unavyozingatiwa hasa kwa madhumuni ya kupasha habari au kupitisha ujumbe.

Katika makala hii, mhimili wa pili na wa tatu ilitumika katika uchanganuzi wa matini ya waandishi mbalimbali wa Sarufi ya Kiswahili ili kudhihirisha jinsi wanavyoisuka lugha yao kwa kuzingatia sheria za lugha husika. Kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi ya yaliyomo, tulichambua matini ya waandishi wa Sarufi ya Kiswahili katika muktadha wa ufundishaji na ujifunzaji wa Sarufi ya Kiswahili. Matumizi ya mihimili hii yalitusaidia kushughulikia lengo la utafiti huu ambalo liliangazia kupambanua tofauti za kimaelezo miongoni mwa waandishi wa Sarufi ya Kiswahili. Hapa tulitaka kujua je, lugha inasukwa vipi katika matini ya Sarufi ya Kiswahili kwa kuzingatia sarufi amilifu? Je, tofauti za kimaelezo miongoni mwa waandishi wa Sarufi ya Kiswahili zinasababishwa na utendaji tofauti wa Sarufi ya Kiswahili? Je, upeo wa muachano wa kimawazo unasababishwa na matumizi tofauti ya lugha miongoni mwa waandishi wanapoeleza vipengele vya Sarufi ya Kiswahili? Haya ndiyo baadhi ya maswali yaliyotuchochea kutumia Sarufi Amilifu.

Nadharia ya pili katika makala hii ni Nadharia ya Ujifunzaji Kitajiriba ya David Allen Kolb (1984). Nadharia hii inaegemea tajiriba kama kigezo kikuu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Kati ya mihimili yake sita, tulitumia mmoja ambao ni:

Ufundishaji na ujifunzaji unahitaji kusuluhisha migogoro miongoni mwa binadamu na mazingira. Mhimili huu una dhana kwamba, migogoro, tofauti na kutokubaliana ndizo nguzo zinazokuza mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Katika hatua za ufunzaji na ujifunzaji, hali hii humfanya binadamu kurejelea alikoanzia na anakoelekea na kutafuta suluhu kupitia ujuzi wa kufikiria.

**Sampuli na Usampulishaji**

Tulirejelea vitabu 14 katika uchambuzi wa matini ya waandishi wa Sarufi ya Kiswahili. Tuliteua

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.335

vitabu hivi kimakusudi kwa sababu vinatumika katika shule za upili nchini Kenya. Vitabu hivi ni:

- Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha 1
- Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha 2
- Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha 3
- Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha 4
- Chemchemi ya Kiswahili Kidato cha 2
- Chemchemi ya Kiswahili Kidato cha 3
- Chemchemi ya Kiswahili Kidato cha 4
- Uhondo wa Kiswahili Kidato cha 1
- Kiswahili Fasaha Kidato cha 1
- Kiswahili Fasaha Kidato cha 3
- Ijaribu na Uikarabati
- Golden Tips
- Longman
- Tanzu za Lugha

## Uchambuzi wa Maelezo Kinzani ya Sarufi ya Kiswahili katika Vitabu Teule vya Shule za Upili Nchini Kenya

Makala hii iliangazia maelezo kinzani katika kazi za baadhi ya waandishi wa Sarufi ya Kiswahili. Tulichambua matini katika vitabu mbalimbali vya Sarufi ya Kiswahili kwa madhumuni ya kudhihirisha vipengele tata. Waaidha, tulizingatia mada mahususi za Sarufi ya Kiswahili ambazo ni: Vitenzi, uainishaji wa sauti /j/, uainishaji wa maneno (nomino) na uchambuzi wa virai.

## Tofauti za Kimaelezo kuhusu Vitenzi vya Kiswahili

Tuliangazia mada ya vitenzi katika Sarufi ya Kiswahili kwa kuchunguza namna ambavyo waandishi wa Sarufi ya Kiswahili wanavyovizungumzia. Tuliegemea vigezo vitatu: Fasili za waandishi hususan maana za dhana, uainishaji kiidadi na ufafanuzi kimuundo. Tulianza kwa kuchambua matini ya Vonyoli na wenzake (2018) kuhusu uainishaji wa vitenzi. Waandishi hawa ndio waliandika kitabu cha *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Pili.* Waliainisha vitenzi vya Kiswahili kama ifuatavyo:

- Vitenzi halisi
- Vitenzi vikuu
- Vitenzi visaidizi
- Vitenzi vishirikishi vipungufu
- Vitenzi vishirikishi vikamilifu
- Vitenzi sambamba

(Vonyoli na wenzake, 2018:78)

Kutokana na dondoo hili, kuna aina sita (6) za vitenzi. Kwa hivyo, kulingana na mtazamo wa waandishi hawa, vitenzi vya Kiswahili vimegawika katika makundi sita. Kwa hivyo, hii ndiyo orodha maalumu ya vitenzi kwa mujibu wa Vonyoli na wenzake (2018). Suala la orodha maalumu katika Sarufi Amilifu kama ilivyogusiwa na Dik (1978) ni kwamba, vipengele vya lugha hupangwa katika orodha maalumu kwa ajili ya kuelewa sarufi ya lugha husika. Kupitia kazi za waandishi katika vitabu, mwelekeo kuhusu ufundishaji na ujifunzaji hutolewa. Mwelekeo wa aina hii ndio uliangaziwa na msomi O'neill (1982) alipohoji kuwa, katika ufundishaji na ujifunzaji wa kisasa, vitabu hutoa mwelekeo mwafaka kwa mwalimu na wanafunzi. Kwa mujibu wa uchunguzi wetu, mwelekeo unaowasilishwa na Vonyoli na wenzake (2018) kuhusu idadi ya aina ya vitenzi ni kuwa, vipo aina sita kuu ya vitenzi katika Sarufi ya Kiswahili.

Kwa upande mwingine, Wamitila na Waihiga (2003) katika kitabu chao cha kiada cha *Chemchemi ya Kiswahili Kidato cha Pili* wana uainishaji ufuatao:

Vitenzi huweza kugawika katika makundi mawili makuu:

- Vitenzi halisi (T)
- Vitenzi vishirikishi (t)

(Wamitila na Waihiga, 2010: 173)

Kwa mujibu wa mifano hii, waandishi wamevigawa vitenzi katika makundi mawili makuu. Makundi haya ni vitenzi halisi na vitenzi vishirikishi. Orodha hii ni kinyume na ile ya Vonyoli na wenzake (2018) katika *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Pili* ambao walitambua aina sita (6) za vitenzi. Hapa hivi tunaona kwamba, waandishi hawa wametofautiana kwa kuzingatia kigezo cha uainishaji kiidadi. Hii inadhihirisha ukinzani kiidadi kuhusu kipengele cha vitenzi miongoni mwa waandishi wanaoandika vitabu vinavyopaswa kuwaongoza walimu na wanafunzi katika ufunzaji na ujifunzaji.

Tulipoelekeza darubini yetu katika kitabu cha *Johari ya Kiswahili Kidato cha Pili*, tulipata kwamba, aina kuu za vitenzi ambazo

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.335

zimetambuliwa na waandishi wake ni tatu (3). Hizi ni:

- Vitenzi halisi
- Vitenzi vikuu
- Vitenzi visaidizi

(Mumbo na Ngamia, 2003:67).

Kwa mujibu wa mifano hii, waandishi wametambua aina tatu (3) za vitenzi. Orodha hii inakinzana na ya Wamitila na Waihiga (2010) yenye makundi mawili (2) na ile ya Vonyoli na wenzake (2018) yenye aina sita (6).

Isitoshe, nao Ipara na Waititu (2011) katika kitabu chao cha ziada cha *Ijaribu na Uikarabati* wanaonesha kwamba kuna aina tano (5) za vitenzi katika Kiswahili.

Aina hizi ni:

- Vitenzi halisi
- Vitemzi vikuu
- Vitenzi visaidizi
- Vitenzi vishirikishi
- Vitenzi sambamba

(Ipara na Waititu, 2011:47).

Kutokana na mifano iliyoteuliwa, tuligundua kwamba, waandishi hawa wana mtazamo kwamba, kiidadi, aina za vitenzi ni tano (5). Mtazamo huu ni kinyume na ule wa Vonyoli na wenzake (2018) waliotuonesha kuwa aina za vitenzi ni sita (6). Tukirejelea orodha zao kama zilivyowasilishwa, tunaona kwamba idadi hii inatofautiana kutokana na mgawanyo wa vitenzi vishirikishi. Vonyoli na wenzake (2018) wamevitenga vitenzi vishirikishi katika aina zake ndogo ambazo ni vitenzi vishirikishi vikamilifu na vitenzi vishirikishi vipungufu. Nao Ipara na Waititu (2011) katika orodha yao hawajavigawa vitenzi vishirikishi katika aina zake ndogo.

Aidha, Mumbo na Ngamia (2003) katika kitabu cha *Johari ya Kiswahili* wana aina tatu (3) ya vitenzi. Katika orodha hiyo, hakuna vitenzi vishirikishi. Kulingana na Mumbo na Ngamia (2003), aina hizi tatu (3) ni vitenzi halisi, vitenzi vikuu na vitenzi visaidizi. Nao Wamitila na Waihiga (2010) wanatambua makundi mawili ya vitenzi. Makundi haya ni: Vitenzi halisi na vitenzi vishirikishi.

Tofauti hizi kuhusu idadi ya aina za vitenzi zinadhihirisha kuwa, waandishi mbalimbali wana mitazamo inayokinzana kuhusu uainishaji wa vitenzi kiidadi. Katika ufundishaji na ujifunzaji wa Sarufi ya Kiswahili, silabasi ndiyo mwelekeo thabiti unaoweza kuondoa hali ya mikinzano kama hii. Tuliporejelea silabasi ya Kiswahili ya KIE (2002), vitenzi vimeainishwa hivi:

- Vitenzi halisi
- Vitenzi vikuu
- Vitenzi visaidizi
- Vitenzi vishirikishi vipungufu
- Vitenzi vishirikishi vikamilifu
- Vitenzi sambamba

(Asili: Silabasi ya Kiswahili ya KIE, 2002:37)

Kulingana na mifano hii kutoka silabasi ya Kiswahili ya Taasisi ya Elimu ya Kenya (KIE, 2002), vitenzi vya Kiswahili vimegawika katika makundi sita. Huku kutofautiana kiidadi kwa waandishi mbalimbali kunawakanganya wanafunzi hususan watahiniwa wakati swali linapotungwa idadi ya aina ya vitenzi. Kuna wale ambao huenda wakataja kwamba kuna aina tano (5) kama wanavyodai Ipara na Waititu (2011). Wengine wanatambua aina sita (6) kama wanavyosema Vonyoli na wenzake (2018). Isitoshe, wengine huenda wakaorodhesha zile aina tatu (3) za vitenzi kwa mujibu wa Mumbo na Ngamia (2003). Si ajabu wengine wakishikilia msimamo kwamba kuna makundi mawili tu ya vitenzi kama wanavyodai Wamitila na Waihiga (2010) ambayo ni vitenzi halisi na vitenzi vishirikishi.

Tulipowauliza wanafunzi kuhusu jinsi tofauti kama hizi zinavyowatatiza, asilimia 78% (N=90) walidai kwamba, wanashindwa kupata msimamo au mwelekeo faafu kuhusu baadhi ya uwasilishwaji wa mada za sarufi hususan vitenzi katika Sarufi ya Kiswahili. Dai hili kutoka kwa wanafunzi lilituwezesha kupata habari kwamba, ufunzaji na ujifunzaji unalemazwa na tofauti za idadi ya vitenzi miongoni mwa waandishi.

Tuliwasaili watafitiwa wanafunzi kuhusu maoni yao kuhusiana na tofauti kiidadi kuhusu vitenzi kama inavyojitokeza katika kazi za waandishi kama vile Vonyoli na wenzake (2018) na Wamitila na Waihiga (2010). Matokeo yakawa, asilimia 78% (N=90) ya wanafunzi wanatatizika kwa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.335

kuchanganyikiwa katika uelewekaji wa Sarufi ya Kiswahili kutokana na tofauti ya aina hii (rejelea kiambatisho cha 3). Hivyo basi, utafiti wetu ulibaini kuwa, kutatizika huku kunafanya baadhi ya vitabu visiwafaidi wanafunzi kwa kukosa kukidhi mahitaji yao. Mtazamo wa asilimia 78% (N=90) ya wanafunzi wanaotatizika kutokana na maelezo kinzani ilithibitisha kauli ya Landrum na wenzake (2012) waliodai kwamba, maoni ya wanafunzi kuhusu vitabu wanavyosoma husaidia kukidhi mahitaji yao. Hapa hivi, mitazamo kinzani inapotokea, baadhi ya mahitaji yao katika uelewekaji wa Sarufi ya Kiswahili hayatimizwi. Maoni yetu ni kwamba, tofauti za aina hii zinapotokea, walimu na wanafunzi warejelee mwelekeo uliowekwa kwenye silabasi ya Kiswahili. Silabasi ya Kiswahili ya Taasisi ya Elimu ya Kenya inayoelekeza kwamba, aina za vitenzi ni sita (K.I.E, 2002).

Tulipowahoji walimu wanaofunza Sarufi ya Kiswahili katika kidato cha nne, walimu 10 (83%) kati ya 12 walitueleza kuwa, tofauti za kiidadi kama hizi huwatatiza wanapoandaa maazimio ya kazi na andalio la somo. Kwa mfano, kuna wale wanaoweza kuandaa maazimio ya kazi yanayoonesha kwamba kuna aina 6 za vitenzi ilhali wengine wakaandaa yenye aina 5 za vitenzi. Hapa hivi tunaona kwamba kuna mgogoro baina ya waandishi ambao unatokana na tofauti za kimawazo baina yao. Ili kusuluhisha mgogoro wa aina hii, tajiriba ndiyo silaha anavyotusisitizia Kolb (1984) kupitia mhimili wa tatu wa nadharia ya Ujifunzaji Kitajiriba anapodai kwamba, ufundishaji na ujifunzaji unahitaji kusuluhisha migogoro miongoni mwa binadamu na mazingira. Kolb (1984) kupitia mhimili huu alidokeza kwamba, migogoro humfanya binadamu arejelee alikoanzia na anakoelekea ili kutafuta suluhu kupitia ujuzi wa kufikiria.

Katika uchunguzi wetu, tuliwahoji walimu wa Sarufi ya Kiswahili kuhusu jinsi wanavyotumia tajriba yao kukabiliana na migogoro miongoni mwa waandishi. Mojawapo ya mbinu waliyotueleza ni, kuwaalika wataalamu wa Sarufi wenye tajirba pevu kuwazungumzia wanafunzi kuhusu dhana zinazosababisha migogoro mathalan idadi maalumu ya vitenzi katika Sarufi ya Kiswahili. Wataalamu hawa wana uwezo wa kufafanua sehemu katika Sarufi ya Kiswahili zilizo na utata kwa vile wana ujuzi wa kufikiria kama asemavyo Kolb (1984) katika mhimili wa tatu anaposema, binadamu hurejelea alikoanzia na anakoelekea kwa kutafuta suluhu kupitia ujuzi wa kufikiria.

Ilibainika kwamba, waandishi tofauti wana mitazamo tofauti kuhusu uainishaji wa vitenzi. Hili huenda linatokana na waandishi hawa kuwa na tajiriba na uzoefu unaotofautiana. Tofauti hizi ndizo zinasababisha migogoro. Ili kusuluhisha migogoro ya aina hii, Kolb na Kolb (2011) wakizungumzia nadharia ya Ujifunzaji Kitajiriba wanapendekeza kwamba, tajiriba pia inaweza kutumika kusuluhisha migogoro. Tajiriba hii inasuluhisha migogoro kupitia ukomavu wa maarifa anayopata mtu. Maoni haya ya Kolb na Kolb (2011) yalitufaa katika utafiti wetu kwa njia ifuatayo, yalituchochea kuwasaili walimu wa Sarufi ya Kiswahili wanavyotumia tajiriba kusuluhisha tofauti za kimaelezo miongoni mwa waandishi wa Sarufi ya Kiswahili. Tuligundua kwamba, walimu wenye tajiriba pana wanatumia fasili zao kwa kutengeneza matini changamani inayopunguza mikanganyo itokanayo na mitazamo kinzani ya waandishi wa Sarufi ya Kiswahili.

Tulipochambua matini katika kitabu cha *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Pili*, tulipata maelezo kuhusu maana ya kitenzi/vitenzi visaidizi ambayo ilizua mtazamo kinzani kwa mujibu wa fasili za waandishi ikilinganishwa na maelezo katika vitabu vingine. Maelezo haya ni kama yafuatayo:

Vitenzi visaidizi hutumika pamoja na vitenzi vikuu au halisi ili kuwasilisha ujumbe. Vitenzi hivi huchukua viambishi mwanzoni tu. Vitenzi visaidizi hutangulia vitenzi vikuu au vitenzi halisi wakati wowote katika sentensi. Aghalabu, vitenzi hivi ndivyo hudhihirisha vyeo (hali au nyakati) za tendo. (Vonyoli na wenzake, 2018:81).

Kwa mujibu wa fasili hii, vitenzi visaidizi huchukua viambishi mwanzoni pekee. Aidha, vitenzi visaidizi huja kabla ya kitenzi halisi au kitenzi kikuu. Tulizamia katika kuchambua matini katika vitabu vingine vya kiada na ziada hususan kubaini maelezo yaliyotolewa kuhusu kitenzi kisaidizi. Kulingana na maelezo haya, tulielekeza darubini yetu kwenye sentensi ya pili ambayo kwa mujibu wa fasili ya waandishi hawa, kuna tofauti za kimaelezo kuhusu ufafanuzi wa dhana ya kitenzi kisaidizi. Tuling'amua kwamba, sentensi hii ina mtazamo unaoleta ukinzani kifasili. Hii ni kwa sababu vitenzi visaidizi huwa na viambishi awali na viambishi

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.335

tamati na wala si viambishi vya mwanzoni tu kama wanavyosema Wamitila na Waihiga (2003). Hapa, maelezo wanayotoa Wamitila na Waihiga (2003) yanatusaidia kuthibitisha kwamba maelezo ya akina Vonyoli na wenzake (2018) yanakanganya wanapozungumzia kuhusu viambishi. Wamitila na Waihiga (2003) wanasema, viambishi ni viungo vyenye maana ambavyo hufungamanishwa na mzizi wa neno ili kulipa neno hilo maana mbalimbali. Wasomi hawa waliainisha viambishi katika makundi mawili ambayo ni: Viambishi awali na viambishi tamati. Kwa mfano, tazama sentensi ifuatayo:

- Baba *alikuwa* analima shambani.

(Mfano wetu)

Katika sentensi hii, neno *alikuwa* ni kitenzi kisaidizi chenye viambishi vifuatavyo, *a*-*li*-*ku*-**w**-*a*. Hapa hivi, a-, li-, na ku- ni viambishi awali huku –a kikiwa ni kiambishi tamati. Maelezo haya yanaifanya ile dhana katika *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Pili* kwamba vitenzi visaidizi huchukua viambishi mwanzoni tu iwe tofauti katika maelezo yaliyomo kwa kuzingatia kigezo cha fasili za waandishi wake. Hapa, waandishi hawa wameibuka na matini ambayo yanavuruga uelewekaji wa vitenzi visaidizi.

Tumeona kwamba wakati ambapo Vonyoli na wenzake (2018) wanadai kwamba vitenzi visaidizi huchukua viambishi mwanzoni tu, akina Wamitila na Waihiga (2003) nao wanadai kwamba, vitenzi visaidizi huchukua viambishi mwanzoni na vilevile mwishoni mwa mzizi wake. Utokeaji wa matini kama hii inayokanganya katika vitabu vya Sarufi ya Kiswahili, kunavifanya vitabu hivi kutotosheleza mahitaji ya walimu na wanafunzi. Hii inathibitisha kauli ya Tomlison (1998) na Richards (2001) waliodai kwamba, hakuna kitabu kimoja ambacho kinatosheleza mahitaji yote ya mwanafunzi au mwalimu. Hali hii huwafanya walimu kuandaa matini mseto kutoka kutoka vitabu mbalimbali. Kuhusiana na hili, uchunguzi wetu ulibaini kwamba, asilimia 67% (N=8) ya walimu huunda matini mapya kwa kupitia kazi mbalimbali za waandishi.

Ingawa Kiai na Maroko (2013) walidai kwamba, uteuzi wa matumizi ya vitabu tofautitofauti katika somo unasababisha mwalimu kushindwa kufafanua maelezo kinzani, sisi tulitofautiana na kauli yao kwa misingi kwamba, mwalimu ana tajiriba kama msomi aliyehitimu kozi ya ualimu. Isitoshe, mwalimu ana silabasi ya Kiswahili kama mwongozo unaomwauni kuandaa matini yake. Kwa mfano, silabasi ya Kiswahili ya Taasisi ya Elimu ya Kenya (KIE, 2002) inaelekeza kwamba, viambishi vya Kiswahili vina muundo wa viambishi awali na viambishi tamati. Silabasi hii ndiyo chombo kinachodhibiti ufundishaji na ujifunzaji wa Sarufi ya Kiswahili. Licha ya silabasi hii kutoa mwongozo wa ufundishaji na ujifunzaji wa Sarufi ya Kiswahili, walimu hukuza matini yao kupitia tafiti na kudurusu makala mbalimbali kwa kusudi la kuimarisha ufundishaji wao kama walivyotueleza tulipowahoji. Kwa kufanya hivyo, mwalimu hufanya utafiti wake mapema ili kutambua ufafanuzi wa maelezo yaliyomo katika vitabu tofauti kama wasemavyo Abai na Nyandiba (2019).

### Tofauti za Kimaelezo kuhusu Dhana ya Vitenzi Halisi

Katika uchambuzi wetu tuling'amua kuwa, maelezo yanayotolewa kuhusu vitenzi halisi miongoni mwa waandishi wa Sarufi ya Kiswahili yanatofautiana. Kwa kuzingatia kigezo cha maana za dhana tulipata kwamba Wamitila na Waihiga (2003) katika *Chemchemi ya Kiswahili Kidato cha Pili*, wana maelezo yafuatayo kuhusu kitenzi halisi:

Kitenzi halisi huweza kutokea katika mfululizo wa vitenzi sambamba ambapo kimoja huwa kitenzi kikuu (T) na vingine ni vitenzi visaidizi (Ts). (Wamitila na Waihiga, 2003: 173).

Kutokana na kifungu hiki, kitenzi halisi ni kitenzi ambacho hutokea katika mfuatano wa vitenzi sambamba.

Mifano ambayo imetolewa ni:

- Mama <u>amekwenda</u> kondeni.
  T
- Panya <u>ameshikwa</u> na paka.
  T
- Nyoka <u>amemuuma</u> ngamia yule.
  T
- Kitabu chake <u>kimeraruka</u>.
  T
- Wakulima <u>wamevuna</u> mahindi mengi.
  T

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.335

(Wamitila na Waihiga, 2003:173)

Kulingana na tungo katika dondoo hili, vitenzi halisi hapa ni amekwenda, ameshikwa, amemuuma, kimeraruka na wamevuna. Vitenzi hivi vyote vimetokea kama kitenzi kimoja tu katika utungo. Tulipochunguza zaidi kuhusu maelezo ya kitenzi halisi, tulibaini kuwa, Wamitila na Waihiga (2003) wanakitambua kitenzi halisi kama kitenzi kisaidizi. Hali hii inatokea katika tungo zenye vitenzi sambamba. Vitenzi sambamba ni vitenzi ambavyo hufuatana moja kwa moja katika sentensi. Maelezo yao ni kwamba:

Kitenzi halisi huweza kutokea katika mfululizo wa vitenzi sambamba ambapo kimoja huwa kitenzi kikuu (T) na vingine ni vitenzi visaidizi (Ts). (Wamitila na Waihiga, 2003: 173)

Ufafanuzi kuhusu kitenzi halisi kutokana na dondoo hili ni kwamba, katika safu ya vitenzi sambamba, vipo vitenzi halisi vinavyotokea katika mfululizo huo. Sentensi ambazo zilitolewa kama mifano kwa mujibu wa maelezo haya ni:

- Jana asubuhi nilikuwa nikiandika barua.
  Ts T
- Kaloki alikuwa anataka kunishambulia.
  Ts Ts T
- Mwanafunzi anapaswa kusoma kwa bidii.
  Ts T
- Sungura wangu angali anakula majani.
  Ts T
- Sisi tumewahi kutembelea mji wa Dar es Salaam. Ts T

(Wamitila na Waihiga, 2003:173)

Kulingana na kifungu hiki, katika sentensi ya (i) …*nilikuwa nikiandika* ndivyo vitenzi sambamba (vinavyofuatana). Kwa hivyo, …*nilikuwa* ni kitenzi halisi huku …*nikiandika* kikiwa ni kitenzi kikuu. Hata hivyo, sisi hatukuridhika na ufafanuzi huu. Mtazamo wetu ni kwamba, hakuna kitenzi halisi katika sentensi ya (i) kama wanavyodai Wamitila na Waihiga (2003). Kwa mfano, tulivichukulia vitenzi **nilikuwa** katika sentensi ya (i), **angali** katika (iv) na **tumewahi** katika (v) kuwa vitenzi visaidizi. Hii ni kwa misingi kwamba vinatokea kabla ya vitenzi vingine katika sentensi.

Tulizamia uchambuzi zaidi wa matini ya wataalamu wengine wa Sarufi ya Kiswahili. Mojawapo ya kazi tulizochunguza ni ya Ipara na Waititu (2011) katika kitabu chao kiitwacho *Ijaribu na Uikarabati*. Baada ya kuchumbuamatini yao, tulibaini kwamba wao wana mtazamo tofauti sana kuhusu vitenzi halisi ikilinganishwa na Wamitila na Waihiga (2003). Wanasema hivi:

Vitenzi hivi (kwa maana ya vitenzi halisi) hujitokeza pekee katika sentensi. (Ipara na Waititu, 2011: 47).

Kutokana na maelezo haya, kitenzi halisi hutokea kama kitenzi kimoja tu katika utungo. Pia, kitenzi halisi kinajitosheleza kimaana. Hii ni tofauti na mtazamo wa Wamitila na Waihiga (2003) wanaokiona kitenzi halisi kama kitenzi ambacho kinaweza kutokea katika mfululizo wa vitenzi vingine katika sentensi. Ipara na Waititu (2011) wanatetea msimamo wao kupitia mifano yao ya sentensi zenye vitenzi halisi kama ifuatavyo:

- Ndege ametaga yai.
- Mkurugenzi ameteuliwa.
- Amiri jeshi hukagua gwaride.
  (Ipara na Waititu, 2011: 47)

Kwa mujibu wa mifano hii, maneno yaliyopigiwa mstari, yaani *ametaga*, *ameteuliwa* na *hukagua* ndiyo vitenzi halisi. Kulingana na wao, vitenzi hivi haviambatani na vitenzi vingine katika utungo. Vinatokea kama kitenzi kimoja tu katika sentensi. Huu ndio msimamo wa Ipara na Waititu (2011) kuhusu vitenzi halisi.

Tuliporejelea mtazamo wa Vonyoli na wenzake (2018) katika kitabu cha *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Pili*, tulipata kwamba wao wana mtazamo sawa na akina Ipara na Waititu (2011). Tulinakili mifano ya tungo zenye vitenzi halisi kwa mujibu wa Vonyoli na wenzake (2018). Mifano hii ni:

- Sisi tutalima shamba letu.
- Mimi ninakula chakula kitamu.
- Paka amemkamata panya.

(Vonyoli na wenzake, 2018: 79)

Kwa mujibu wa mifano hii, vitenzi *tutalima*, *ninakula* na *amemkamata* ndivyo vitenzi halisi kama wasemavyo Vonyoli na wenzake (2018).

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.335

Muachano huu wa kimawazo kuhusu kitenzi halisi kati ya Wamitila na Waihiga (2003), Ipara na Waititu (2011) na Vonyoli na wenzake (2018), ni mifano ya vipengele tata katika Sarufi ya Kiswahili. Utata huu unatokana na namna ambavyo mwandishi anatoa maelezo yake kwa kutumia lugha. Matumizi haya ya lugha ndiyo yanaangaziwa katika nadharia ya Sarufi Amilifu kupitia mhimili wa tatu unaorejelea matini yanavyosukwa katika lugha.

Katika nadharia hii, Dik (1978) alihoji kuwa, ndani ya matini anayowasilisha mwandishi, kuna lugha ambayo ni malighafi inayofanikisha mawasiliano kupitia habari, maandishi, ishara na makala anuwai. Hivyo basi, waandishi mbalimbali huisuka lugha katika matini yao kwa kutumia ujuzi au upekee wao. Ujuzi huu unarejelewa na Dik (1978) kama uamilifu halisi wa lugha. Kwa hivyo, tofauti miongoni mwa waandishi wa Sarufi ya Kiswahili zinachangiwa na namna ambavyo waandishi hawa wanavyoifasiri na kuitumia lugha kwa sababu wao pia wamepata maarifa tofautitofauti kuhusu Sarufi ya Kiswahili katika miktadha tofauti kama vile shule na vyuo walikosomea. Suala la muktadha katika nadharia ya Sarufi Amilifu limepewa kipaumbele kwa misingi kwamba, muktadha huathiri lugha kiutendaji na athari hii husababisha tofauti katika maelezo ya vipengele vya sarufi miongoni mwa waandishi wa sarufi kijumla.

Uchunguzi wetu ulibaini kuwa, walimu wa Sarufi ya Kiswahili wanapoandaa matini yao, wao hutumia ujuzi na tajiriba waliyo nayo kusawazisha mitazamo kinzani ya waandishi na kuibuka na matini changamano. Wanapofanya hivyo, wanasuluhisha migogoro miongoni mwa waandishi kwa kutumia ujuzi na tajiriba yao. Wakati ambapo migogoro hii inasuluhishwa, matumizi ya mhimili wa tatu wa nadharia ya Ujifunzaji Kitajiriba unaosema, ufundishaji na ujifunzaji unahitaji kusuluhisha migogoro miongoni mwa binadamu na mazingira yanabainika.

Kwa maoni yetu, ingawa maelezo ni mengi yanayotofautiana kuhusu dhana ya vitenzi halisi, walimu wanapaswa kuelekezwa na silabasi ya Taasisi ya Elimu ya Kenya (KIE, 2002) ambayo hutoa mwelekeo sawa kwa walimu na wanafunzi wote nchini kuhusu mambo ya kufundishwa.

3.4.2 Tofauti za Kimaelezo kuhusu Viwakilishi vinavyotumika Kuashiria Vitenzi Visaidizi

Uchunguzi wetu uliweza pia kuangazia viwakilishi vinavyotumika kuashiria aina za vitenzi katika Sarufi ya Kiswahili. Uchambuzi wetu wa matini ya kazi za waandishi mbalimbali wa Sarufi ya Kiswahili ulithibitisha kuwepo kwa mitazamo tofauti kuhusu vifupisho rejelewa. Tulianza kwa kudurusu kazi ya Mumbo na Ngamia (2003) katika kitabu chao cha *Johari ya Kiswahili Kidato cha Pili*. Katika kitabu hiki kuna mifano ya sentensi zifuatazo:

- Mtoto <u>alikuwa</u> akilia.<br>ts
- Yaya <u>alikuwa</u> akitafuta kiberiti.<br>ts
- Mkulima <u>aliweza</u> kupanda mahindi.<br>ts
- Mimi <u>sijawahi</u> kuenda Nairobi.<br>ts
- Mwalimu mkuu <u>angali</u> analima.<br>ts

(Mumbo na Ngamia, 2003:68)

Kutokana na mifano katika sentensi hizi, vitenzi visaidizi ni maneno ambayo yamepigiwa mstari yakiwa ni (i) alikuwa, (ii) alikuwa, (iii) aliweza, (iv) sijawahi na (v) angali. Ili kuashiria vitenzi hivi, Mumbo na Ngamia wametumia ishara ya *ts* kama tulivyoinukuu moja kwa moja.

Naye Wamitila (2015) katika kitabu chake cha *Chemchemi ya Kiswahili Kidato cha Nne* ana mtazamo huo huo kupitia tungo zifuatazo:

- Zuberi *alikuwa (ts) akienda (ts) kuwinda (T)*.
- Kamene *alikuwa (ts) anataka (ts) kujiandaa (ts) kupika (T)*.
- Wewe *utakuja (ts) kujuta (T).*

(Wamitila, 2015: 41).

Kifungu hiki kinaonesha kwamba, vitenzi visaidizi katika (a), (b) na (c) vimeoneshwa kwa kutumia kiwakilishi *ts.* Hapa hivi, Wamitila (2015) na Mumbo na Ngamia (2003 wana mtazamo sawa kwamba katika kutambua kitenzi kisaidizi katika utungo, ishara ya *ts* inapaswa kutumika.. Tulichukulia kwamba viwakilishi Ts na ts vinatofautiana kwa misingi ya herufi kubwa katika *Ts.* Mifano katika *Chemchemi ya Kiswahili Kidato cha Nne (Wamitila, 2015)* inakinzana na ile katika

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.335

*Chemchemi ya Kiswahili Kidato cha Pili (Wamitila na Waihiga, 2003)* ambapo kuna sentensi zifuatazo:

- Jana asubuhi nilikuwa nikiandika barua.
  Ts T
- Kaloki alikuwa anataka kunishambulia.
  Ts T
- Mwanafunzi anapaswa kusoma kwa bidii.
  Ts T
- Sungura wangu angali anakula majani.
  Ts T
- Sisi tumewahi kutembelea mji wa Dar es Salaam. Ts T

(Wamitila na Waihiga, 2003:173)

Katika kifungu hiki, waandishi hawa wametumia kiwakilishi cha *Ts* katika kuonesha kitenzi kisaidizi. Hali hii inawaacha wanafunzi katika hali ya suintafahamu kwa sababu kuna vitabu ambavyo vinaashiria vitenzi sambamba kwa alama zile zile za *ts*. Kwa mfano, katika *Chemchemi za Kiswahili Kidato cha Nne*, viwakilishi vya vitenzi sambamba vilivyotumika ni *ts* na *T*. Katika kitabu hicho, *ts* ni kiwakilishi cha kitenzi kisaidizi kama ilivyo katika sentensi zilizotolewa kama mifano ya vitenzi sambamba kutoka kwa *Chemchemi ya Kiswahili Kidato cha Nne* ambazo ni:

- Zuberi alikuwa (ts) akienda (ts) kuwinda (T).
- Kamene alikuwa (ts) anataka (ts) kujiandaa (ts) kupika (T).
- Wewe utakuja (ts) kujuta (T). (Wamitila, 2015: 41)

Kwa mujibu wa mifano hii, mwandishi ametumia kiwakilishi *ts* kuonesha kitenzi kisaidizi ambacho ni alikuwa (ts) katika sentensi ya (i). Aidha, katika sentensi ya (ii) vitenzi visaidizi ni alikuwa (ts), anataka (ts) na kujiandaa (ts). Hatimaye katika utungo wa (iii) kitenzi kisaidizi ni atakuja (ts). Kwa hivyo, kutokana na mifano hii, tulibaini kwamba, waandishi wana mitazamo inayokinzana kuhusu kiwakilishi cha kitenzi kisaidizi; kuna wanaotumia ts na wengine Ts. Hapa, pana uwezekano kuwa Wamitila (2015) anarekebisha makosa ya akina Wamitila na Waihiga (2003). Tuliangazia maoni ya walimu wa Sarufi ya Kiswahili kwa dhamira ya kupata mtazamo wao kuhusu viwakilishi vya vitenzi.Tulipowahoji walimu wa Sarufi ya Kiswahili nyanjani, mwalimu mmoja ambaye ni mtahini wa mtihani wa sarufi alitueleza kwamba, dhana ya ishara za aina za maneno kama vile vitenzi hupuuzwa na baadhi ya walimu na wanafunzi.

Alitudokezea kuwa mapuuza haya yanatokana na ishara hizo kuwakanganya kama ilivyo katika kazi mbalimbali za waandishi wa Sarufi ya Kiswahili.

Isitoshe, tulipochunguza matini katika *Golden Tips*, Mogambi (2015) ametumia kiwakilishi cha **T** kuashiria vitenzi sambamba. Sentensi za Mogambi (2015) ni zifuatazo:

- Kamara analia akila.
  T T
- Maria huchechemea anapotembea.
  T T
- Mbwa anakula akibweka.
  T T
- Wachezaji wanacheka wakiruka.
  T T

(Mogambi, 2015: 38)

Kwa mujibu wa mifano hii, mwandishi ameonesha vitenzi sambamba katika maneno ambayo yamepigiwa mstari. Katika sentensi ya (i) kuna kitenzi kisaidizi *analia* ambapo mwandishi ametumia kiwakilishi cha T kukionesha. Hali hii ni sawa katika sentensi ya (ii), (iii) na (iv). Kwa hivyo, vitenzi visaidizi ambavyo vimetokea kama vitenzi sambamba katika sentensi za Mogambi (2015), vimewakilishwa na kiwakilishi cha T**.** Hii ni kinyume na ilivyo katika *Chemchemi ya Kiswahili Kidato cha Nne* ambapo mwandishi wake ametumia kiwakilishi **ts** kama ilivyo katika sentensi hizi:

- Zuberi alikuwa (ts) akienda (ts) kuwinda (T).
- Kamene alikuwa (ts) anataka (ts) kujiandaa (ts) kupika (T).
- Wewe utakuja (ts) kujuta (T).

(Wamitila, 2015: 41).

Kulingana na mifano katika sentensi hizi, waandishi wametumia kiwakilishi **ts** kurejelea vitenzi visaidizi. Kiwakilishi hiki cha **ts** kinatofautiana na cha Mogambi (2015) anayetumia kiwakilishi cha T kama tulivyoeleza hapo juu. Wakati huo huo naye Wamitila (2015) amekitumia kiwakilishi T kurejelea vitenzi vikuu kwa mujibu wa dondoo. Hapa hivi, viwakilishi hivi vinaonesha mitazani inayokinzana. Matumizi ya viwakilishi vya maneno yameangaziwa na wataalamu kama vile Habibu (2017) aliyefafanua kuwa, katika uainishaji wa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.335

miundo ya maneno katika tungo, aghalabu viwakilishi vyake hutumika ili kurahisisha uwakilishaji wake. Kwa hivyo, viwakilishi hivi vinapotumika visivyo huenda vikakosa kurahisisha uwakilishaji wa aina za maneno katika sentensi.

Viwakilishi vya aina ya vitenzi ni ishara ambazo zinafaa kuzingatiwa hasa wakati ambapo vitenzi vinaainishwa katika tungo kama ilivyo katika aina nyingine za maneno. Kwa hivyo, ishara hizi, yaani **Ts** na **ts** zinapovurugwa au kutambuliwa visivyo, itakuwa ni kinyume na sarufi ya lugha ya Kiswahili. Katika utafiti huu, tulipokuwa tukiwahoji walimu wa Sarufi ya Kiswahili, mwalimu mmoja ambaye amekuwa mtahini wa mtihani wa Sarufi ya Kiswahili katika kiwango cha kitaifa kwa takriban miaka kumi alitueleza kuwa, swali linapotahiniwa kuhusu aina za maneno katika tungo, mtahiniwa anatarajiwa kutumia ishara za aina za maneno hayo kwa mujibu wa Sarufi ya Kiswahili kama mojawapo ya uwasilishaji wa majibu unaozingatiwa. Kwa mfano, iwapo mwanafunzi atatumia kiwakilishi cha **Ts** kumaanisha kitenzi kikuu, atanyimwa alama kwa sababu kiwakilishi ambacho kimekubalika ni **T** huku **Ts** kikiwa cha kitenzi kisaidizi. Kwa hivyo, Mogambi (2015) katika kitabu chake cha *Golden Tips* na Wamitila (2015) katika kitabu chake cha *Chemchemi ya Kiswahili Kidato cha Nne* hawakuzingatia viwakilishi vilivyomo katika silabasi ya Kiswahili ya iliyoundwa na Taasisi ya Elimu ya Kenya (KIE, 2002).

Kulingana na uchambuzi wetu, tuliridhia kwamba wakati ambapo waandishi tofauti wanatumia viwakilishi vinavyotofautiana kurejelea vitenzi, basi wanasababisha tofauti za kimaelezo katika usarufishwaji wa Kiswahili. Katika muktadha huu wa kuwepo kwa viwakilishi vinavyotofautiana kuhusu aina za vitenzi huenda usitatize uelewekaji wa Sarufi ya Kiswahili bali unaathiri umilisi wake. Mathalan, mwanafunzi anapotumia kiwakilishi kisichofaa, atanyimwa alama na hali kama hii inadhihaki juhudi za umilisi wa Sarufi ya Kiswahili.

Kulingana na Ujifunzaji Kitajiriba (Kolb, 1984), ufundishaji na ujifunzaji ni mchakato unaojumlisha mazoea kiutendaji. Mchakato huu unadhibitiwa na fikra, hisia na mitazamo ambayo inakuza ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia sheria kupitia tajiriba kutokana na hali ya mtu kiujumla. Kwa hivyo, mazoea ya kiutendaji katika matumizi ya viwakilishi vya vitenzi ni mitazamo na fikra ambazo zikiwakilishwa visivyo zinaendeleza ukinzani ambao unatatiza shughuli za ufundishaji na ujifunzaji wa Sarufi ya Kiswahili.

Tulipohoji walimu wa Sarufi ya Kiswahili ili kupata fikra, maoni, mitazamo yao kutokana na mtagusano wao na waandishi wa Sarufi ya Kiswahili kupitia ufundishaji wa Sarufi ya Kiswahili, walitueleza kwamba, Sarufi ya Kiswahili inafaa kuzingatiwa kila wakati kwa sababu inaegemea sheria zake ambazo zinafaa kutumika katika uelewekaji wake.

Tulichukua hatua ya kurejelea silabasi ya Kiswahili ya Taasisi ya Elimu ya Kenya (KIE, 2002) ili tubaini ni kiwakilishi kipi ambacho kimependekezwa kutumika kuwakilisha kitenzi kisaidizi. Kulingana na silabasi ya Kiswahili ya Taasisi ya Elimu ya Kenya (KIE, 2002) ambayo inatumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa Sarufi ya Kiswahili nchini Kenya, viwakilishi ambavyo vimebainishwa kuwakilisha aina za vitenzi ni kama vifuatavyo:

- Kitenzi Kikuu (T)
- Kitenzi Kisaidizi (Ts)
- Kitenzi Halisi (T)
- Kitenzi kishirikishi (t)

(Asili: Silabasi ya Kiswahili ya Taasisi ya Elimu ya Kenya, 2002)

Kutokana na utaratibu huu wa silabasi (ambayo ndiyo dira katika ufundishaji na ujifunzaji wa Sarufi ya Kiswahili) walimu na wanafunzi wanatarajiwa kuzingatia viwakilishi hivyo katika shughuli za ufundishaji na ujifunzaji wa Sarufi ya Kiswahili. Vilevile, waandishi wanapojiandaa kuandika matini kuhusu Sarufi ya Kiswahili, wana jukumu la kuzingatia yaliyomo katika silabasi ya Taasisi ya Elimu ya Kenya (KIE, 2002). Hatua hii itawafaa kuepuka kuwasilisha dhana ambazo huenda zikasababisha kuchanganyikiwa au kutofautiana kimaelezo miongoni mwa waandishi wa Sarufi ya Kiswahili. Kwa hivyo, ni bayana kwamba, viwakilishi vya **Ts** na **ts** pia vinaonesha mitazamo kinzani kama ilivyo katika vitabu vya kiada na ziada vinavyotumika katika shule za upili nchini Kenya.

## Tofauti za Kimaelezo kuhusu Uainishaji wa Sauti /ɟ/

Sauti /ɟ/ni mojawapo ya konsonanti ghuna (konsonanti nzito kwa kuzingatia utamkaji wake)

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.335

katika Sarufi ya Kiswahili. Sauti hii imeendelezwa kwa kutumia alama za kifonetiki ambazo ni // katika baadhi ya vitabu vya Sarufi ya Kiswahili vinavyotumika katika shule za upili. Licha ya alama za kifonetiki kutumika, yaani; //, ishara ambayo imetumika si ya kifonetiki katika vitabu hivyo. Kwa mfano, katika kitabu cha *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Kwanza,* kuna maelezo yafuatayo:

Mifano ya sauti za konsonanti:

/b/, /ch/, /d/, /dh/, /f/, /g/, /h/, /j/, /k/ na /l/ (Vonyoli na wenzake, 2018:2).

Kwa mujibu wa mifano hii, alama za kifonetiki // zimetumika kuonesha konsonanti za Kiswahili lakini ishara zilizotumika si za kifonetiki kwa mujibu wa Alfabetu ya Kimataifa ya Kifonetiki (rejelea kiambatisho cha 4).

Kwa upande mwingine, baadhi ya waandishi wa Sarufi ya Kiswahili wameziendeleza sauti za Kiswahili kwa kuchanganya matumizi ya alama za kifonetiki (//) na kuziandika katika hali ya kawaida bila alama zozote. Tazama mifano ifuatayo katika kitabu cha Uhondo wa Kiswahili Kidato cha Kwanza:

…nazali zinapotamkwa, hewa itokayo mapafuni hupitia puani. Mifano ni /m/, /n/, /ny/ na /ng'/.

Konsonanti ghuna ni b, d, n, ng, dh, g, gh, j, r, v, z, w, y (Walibora na Wang'endo, 2004:22).

Kulingana na maelezo haya, mifano ya nazali imeendelezwa kwa kutumia alama za kifonetiki //. Wakati huo huo waandishi hawa wameendeleza sauti (j) ikiwa miongoni mwa konsonanti nyingine za Kiswahili bila alama yoyote. Hapa hivi tunaona kwamba, muendelezo wa sauti katika Sarufi ya Kiswahili haujazingatia muendelezo kwa mujibu wa Alfabeti ya Kimataifa ya Kifonetiki (AKIKI). Kwa misingi hii, muendelezo kama vile /j/ katika kitabu cha *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Kwanza* unarejelea sauti (y) kwa mujibu wa AKIKI. Hapa hivi, muendelezo kama huu unavuruga uwasilishaji wa sauti. Kwa hivyo, katika uchunguzi huu, tumetumia alama na ishara za kifonetiki kwa mujibu wa AKIKI kuonesha sauti /j/ (kama ilivyo katika vitabu vya Sarufi ya Kiswahili. Tumeiendeleza hivi: /ɟ/. Tuliangazia maelezo kuhusu uainishaji wa sauti /ɟ/ baina ya waandishi wa Sarufi ya Kiswahili kwa kuchambua kazi zao. Matokeo yake yalikuwa kama ifuatavyo:

Waandishi Walibora na Wang'endo (2004) katika *Uhondo wa Kiswahili Kidato cha Kwanza*, waliainisha konsonanti za Kiswahili katika makundi yafuatayo:

- Vipasuo
- Vipasuo-kwamizo
- Ving'ong'o/nazali
- Vikwamizo
- Vitambaza
- Vimadende
- Viyeyusho.

(Walibora na Wang'endo, 2004:22-23)

Kati ya makundi haya, waandishi hawa walitambua kwamba, kuna vipasuo saba ambavyo ni: /p/ /b/ /t/ /d/ /k/ /g/ na /j/ kama ilivyo katika ukurasa wa 23 ilhali kipasuo-kwamizo ni kimoja tu ambacho ni: /ch/ kama ilivyofafanuliwa katika ukurasa wa 22 na kuoneshwa katika jedwali la ukurasa wa 23. Tazama jedwali hili:

**Konsonanti za Kiswahili**

| **Aina** | **Mahali** | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Midomo | Meno | Ufizi | Midomo na Meno | Kaakaa gumu | Kaakaa laini | Koromeo |
| Vipasuo | p b | | t d | | j | k g | |
| Vizuio kwamiza | | | | | ch | | |
| Vikwamizo | | th dh | s z | f v | sh | kh gh | h |
| Ving'ong'o | m | | n | | ny | ng' | |
| Kitambaza | | | l | | | | |
| Kimadende | | | r | | | | |
| Kiyeyusho | w | | | | y | | |

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.335

(Walibora na Wang'endo, 2004:23)

Kutokana na jedwali hili, sauti /ɟ/ imeainishwa kama kipasuo kinachotamkwa kwenye kaakaa gumu. Hali hii inajitokeza pia katika kitabu cha *Kiswahili Fasaha Kidato cha Kwanza* ambapo Waititu, Ipara na Okaalo (2003) wanasema:

/ɟ/nayo ni **kipasuo** kinachotamkwa wakati ulimi unapopindwa karibu na kaakaa gumu lakini ukiwa karibu na kinywa. (Waititu, Ipara na Okaalo, 2003: 2).

Kwa mujibu wa maelezo haya, mtazamo wa waandishi hawa ni kwamba, sauti /ɟ/ ni kipasuo. Kwa upande mwingine, Vonyoli na wenzake (2018) katika Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Kwanza wana mtazamo tofauti kuhusu sauti /ɟ/. Wao wanadai kwamba sauti /ɟ/ ni kizuiwa-kwamizo. Tazama jedwali hili:

**Uainishaji wa Konsonanti za Kiswahili**

| Aina | Mahali | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Midomo | Meno | Ufizi | Midomo na Meno | Kaakaa gumu | Kaakaa laini | Koromeo |
| Vipasuo | p b | | t d | | | k g | |
| Vizuio kwamiza | | | | | j ch | | |
| Vikwamizo | | th dh | s z | f v | sh | gh | H |
| Ving'ong'o | m | | n | | ny | ng' | |
| Kitambaza | | | l | | | | |
| Kimadende | | | r | | | | |
| Kiyeyusho | w | | | | y | | |

(Vonyoli na wenzake, 2018:3).

Kulingana na jedwali hili, kuna vipasuo sita ambavyo ni: /p/ /b/ /k/ /g/ /t/ /d/ ilhali vizuio-kwamizo ni viwili ambavyo ni: /ch/ na /ɟ/. Vyote vinatamkwa kwenye kaakaa gumu.

Kutokana na mitazamo ya Ipara na Okaalo (2003) na Walibora na Wang'endo (2004), tofauti inayodhihirika hapa kuhusu sauti /ɟ/ ni kuainishwa katika makundi mawili tofauti kwa mujibu wa vitabu hivi ilhali vitabu vyote vinasomwa katika shule za upili nchini Kenya. Tofauti ambayo inasababisha mkinzano katika uainishaji huu inatokana na maelezo waliyotoa waandishi kuhusiana na makundi haya ya sauti. Ufafanuzi huu ulikuwa kama ifuatavyo:

Katika *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Kwanza*, Vonyoli na wenzake (2018) wanasema hivi:

Sauti hizi zinapotamkwa ala husika hugusana kisha hewa iliyozuiliwa huachiliwa ghafla kusababisha mfyatuko au mpasuko. (Vonyoli na wenzake, 2018: 4).

Kutokana na maelezo haya, wakati sauti /ɟ/ inapotamkwa, hewa husababisha mpasuko inapoachiliwa kutoka chemba kinywa. Maana ya maelezo haya kulingana na sisi ni kuwa, sauti /ɟ/ ina mpasuko kama ilivyo katika sauti zingine zenye mipasuko wakati wa utamkaji kama vile /p/, /b/, /k/, /g/, /t/ na /d/. Kwa hivyo, hata kama Vonyoli na wenzake (2018) wametoa maelezo yanayoafiki sauti /ɟ/ kuwa kipasuo, wao wanadai kwamba sauti /ɟ/ ni kizuiwa-kwamizo. Tulizidi kuchunguza maelezo kuhusu sauti /ɟ/ katika *Uhondo wa Kiswahili Kidato cha Kwanza* ambapo Walibora na Wang'endo (2004) wanasema:

Wakati vinapotamkwa (vipasuo) hewa husukumwa kutoka mapafuni kwa nguvu na kuzuiwa kinywani, kisha ikaachiliwa ghafla na kutoa sauti ya kupasuka. (Walibora na Wang'endo, 2004: 22).

Waandishi hawa wana mtazamo kwamba, vipasuo vikitamkwa, hewa hutoka kwa kutoa sauti ya kupasuka. Hii ndiyo sababu wameiainisha sauti /ɟ/ kama kipasuo. Tulipolinganisha ufafanuzi kuhusu sauti ambazo ni vizuiwa kwamiza, waandishi katika

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.335

*Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Kwanza* nao wanavifafanua vizuiwa kwamiza hivi:

Hizi ni sauti ambazo kuna mzuio wa hewa kwa muda mfupi na muachilio wake polepole: /j/, /ch/. (Vonyoli na wenzake, 2018: 4).

Hapa hivi, waandishi hawa wanadai kuwa, sauti /ɟ/ inapotamkwa, hewa huachuliwa polepole bila mpasuko. Hii ndiyo sababu ya wao kuiainisha sauti /ɟ/ kama kizuiwa-kwamizo. Nao Walibora na Wang'endo (2004) katika *Uhondo wa Kiswahili Kidato cha Kwanza*, wanasema haya kuhusu vizuiwa kwamiza:

Vinapotamkwa hewa hupitishwa kwa nguvu kutoka mapafuni na kuzuiwa kinywani. Huwa nafasi ndogo inabakia baina ya viungo vya kutamkia. Mfano ni /ch/. (Walibora na Wang'endo, 2004: 22).

Kwa mujibu wa maelezo haya, waandishi hawa wanadai kwamba vizuio-kwamizo vinapotamkwa, hewa huzuiliwa kinywani; hakuna mpasuko unaotokea. Kulingana na wao, ni sauti /ch/ pekee inayoafiki maelezo hayo.

Tofauti hizi zinadhihirisha kwamba, waandishi katika vitabu hivi wana mtazamo unaokinzana kwa mujibu wa maelezo ya sauti /ɟ/ katika Sarufi ya Kiswahili. Kulingana na Walibora na Wang'endo (2004), sauti /ɟ/ ina sifa za ufafanuzi unaotolewa kuhusu vipasuo na Vonyoli na wenzake (2018). Kuwepo kwa mitazamo kinzani kuhusu sauti /ɟ/ ni kunatokana na kuvurugwa kwa sifa za sauti hii.

Kuna vigezo maalumu ambavyo huzingatiwa tunapoipa sauti sifa bainifu. Ufafanuzi kuhusu sifa hizi unadhirika katika maelezo ya msomi Bruno (2020) ambaye ni mtaalamu wa masuala ya fonolojia na othografia. Anaeleza kwamba, katika mtindo wa sauti za lugha, vigezo maalumu hutumika katika kuainisha sauti za lugha. Bruno (2020) aliangazia vigezo vya kuanisha sauti na kudokeza kwamba, kuna vigezo vitatu ambavyo ni pamoja na mahali pa kutamkia, jinsi ya kutamka konsonanti na hali ya mrindimo wa nyuzi za koromeo. Kwa mfano, kwa mujibu wa vigezo hivi, sauti za /tʃ/ na /ɟ/ zina sifa zifuatazo:

/tʃ/

- Ni kizuio kwamiza.
- Inatamkwa kwenye kaakaa gumu.
- Ina mrindimo mwepesi wa nyuzi za koromeo (ni sighuna).

/ɟ/

- Ni kizuio kwamiza.
- Inatamkwa kwenye kaakaa gumu.
- Ina mrindimo mzito wa nyuzi za koromeo (ni ghuna).

Naye Habibu (2017) alidokeza kwamba katika masuala ya sarufi ya lugha, kutokana na uvumbuzi, utafiti na maoni mapya, huwa kunazuka mambo mapya ambayo ndiyo ishara ya ukuaji wa lugha. Mapendekezo yake Bruno (2020) ni kwamba, hata kama mabadiliko yatatokea katika sarufi ya lugha, inafaa vigezo maalumu vizingatiwe kila mara ili kuzuia kuibuka kwa mikabala chungu nzima katika ufafanuzi wa vipengele vya lugha. Matokeo ya utafiti huu yalionesha kwamba, asilimia 49% (N=56) ya wasailiwa wakiwa ni wanafunzi walidokeza kwamba, tofauti za kimaelezo mathalan sauti /ɟ/ unawatatiza wanaposoma Sarufi ya Kiswahili. Wanashindwa ni mtazamo upi miongoni mwa waandishi ambao ni sahihi katika ufundishaji na ujifunzaji wa baadhi ya vipengele vya sarufi kama vile uainishaji wa sauti /ɟ/iwapo ni kipasuo au kizuio-kwamiza.

Tulirejelea Alfabeti ya Kimataifa ya Kifonetiki (AKIKI, 2020) kwa dhamira ya kubainisha uainishaji wa sauti /ɟ/. Tulifanya hivyo kwa sababu AKIKI hutoa mwelekeo wa kimataifa kuhusu sifa za kifonetiki za sauti ambazo zinatumika katika lugha mbalimbali ulimwenguni. Kwa mujibu wa AKIKI (2020), sauti /ɟ/imeainishwa kama kipasuo kinachotamkwa katika kaakaa gumu (rejelea kiambatisho cha 4).

Maoni yetu ni kwamba, sauti /ɟ/ ni kipasuo. Hii ni kwa misingi kwamba, sauti /ɟ/inapotamkwa, hewa huwachiliwa kwa mlipuko baina ya ala za kutamkia. Nayo Silabasi ya Kiswahili ya Taasisi ya Elimu ya Kenya (KIE, 2002) inayotoa mwelekeo sawa kwa walimu na wanafunzi wote inasema kwamba, sauti /ɟ/ ni kizuiwa-kwamizo.

**Tofauti za Kimaelezo kuhusu Uainishaji wa Nomino za Kiswahili**

Uchunguzi wetu ulishughulikia uainishaji wa baadhi ya nomino za Kiswahili. Dhamira yetu

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.335

ilikuwa ni kubaini iwapo kuna maelezo yanayokinzana kuhusu uainishaji wa baadhi ya nomino. Nia ya kufanya hivi ilikuwa ni kudhihirisha mitazamo tofauti miongoni mwa waandishi wa Sarufi ya Kiswahili kupitia kazi zao. Tuliangazia namna ambavyo waandishi wamezigawa nomino za Kiswahili katika makundi mbalimbali. Baada ya uchambuzi wa kina, tuligundua kwamba kuna maelezo yanayotofautiana miongoni mwa waandishi kuhusu dhana ya nomino za kawaida na nomino za mguso. Matokeo yake ni kama ifuatavyo:

Wasomi Walibora na Wang'endo (2004) katika *Uhondo wa Kiswahili Kidato cha Kwanza*, waliziainisha nomino za Kiswahili katika makundi yafuatayo.

- Nomino za pekee
- Nomino za kawaida
- Nomino za mguso
- Nomino dhahania
- Nomino za jamii

(Walibora na Wang'endo, 2004:15).

Kwa mujibu wa maelezo haya, waandishi wamezigawa nomino katika makundi matano. Kulingana na orodha hii, nomino za kitenzi-jina hazipo ingawaje ni mojawapo ya kundi la nomino katika Sarufi ya Kiswahili kama wanavyodai Vonyoli na wenzake (2018) katika kitabu chao cha *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Pili*. Hii ndiyo orodha yao:

- Nomino za pekee
- Nomino za kawaida
- Nomino za dhahania
- Nomino za jamii
- Nomino za wingi
- Nomino za kitenzi-jina.

(Vonyoli na wenzake, 2018: 18-19).

Hapa hivi, nomino zimegawika katika makundi sita. Kwa hivyo, Walibora na Wang'endo (2004) hawakuzitambua nomino za wingi na nomino za kitenzi-jina kama ilivyo katika orodha ya Vonyoli na wenzake (2018). Hata hivyo, Vonyoli na wenzake (2018) hawajatambua kuwepo kwa kundi la nomino liitwalo nomino za mguso kama watambuavyo Walibora na Wang'endo (2004). Wanasema:

Hizi ni nomino zinazotaja vitu vya kawaida vinavyopatikana kwa wingi duniani na ambavyo si vya pekee. (Walibora na Wang'endo, 2004:15).

Kutokana na maelezo haya, nomino za kawaida hutaja vitu vya kawaida vinavyopatikana kwa wingi duniani. Mifano iliyotolewa ni kama vile, meza, kitanda, jani na wembe. Ufafanuzi wa Vonyoli na wenzake (2018) katika *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Kwanza* ni kwamba, nomino hizi hazianzi kwa herufi kubwa ila tu zinapotumiwa mwanzoni mwa sentensi. Kuhusu nomino za mguso, waandishi wa *Uhondo wa Kiswahili Kidato cha Kwanza* wanadai kuwa, hizi ni aina za nomino zinazoweza kuguswa au kufikiwa na mwanadamu kwa hisia zake tano yaani kusikia kwa masikio, kugusa kwa kidole, kuona kwa macho( au darubini), kunusa kwa pua au kuonja kwa ulimi. Mifano iliyotolewa ni: nyumba, mtu, jiwe, kitabu na kalamu (Walibora na Wang'endo, 2004). Maelezo haya yanafanana na yaliyomo katika kitabu cha *Tanzu za Lugha Kidato cha Nne* ambapo Olodo na Njogu (2005) wanatoa maelezo kuhusu nomino za kawaida kwamba, hujumlisha vitu au vyombo halisi vinavyoonekana na kuguswa. Maelezo katika kitabu cha Olodo na Njogu (2005) yanarejelea nomino za kawaida na wala si nomino za mguso kama zinavyotambuliwa na Walibora na Wang'endo (2004).

Tumethibitisha kwamba kuna mitazamo tofauti kuhusu nomino za kawaida na nomino za mguso. Akina Walibora na Wang'endo (2004) wanapotambua nomino za mguso, Vonyoli na wenzake (2018) nao hawatambui kuwepo kwa nomino za mguso. Kilichopo ni kuwa, maelezo na mifano ya nomino za kawaida kwa mujibu wa Vonyoli na wenzake (2018) yanaafikiana na maelezo ya nomino za mguso kulingana na Walibora na Wang'endo (2004).

Kutokana na utambuzi huu, waandishi wa vitabu hivi vitatu; yaani, *Uhondo wa Kiswahili Kidato cha Kwanza* na *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Kwanza* na *Tanzu za Lugha Kidato cha Nne* wanatofautiana kimawazo jambo linalosababisha mitazamo kinzani katika Sarufi ya Kiswahili katika shule za upili nchini Kenya.

Mtaalamu Richards (2001) anatueleza kwamba, ndani ya matini kwenye vitabu, kuna udhaifu unaosababishwa na waandishi ambao unavuruga ufafanuzi wa matini hayo. Kwa mujibu wa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.335

uchunguzi wetu, kinachosababisha maelezo tata kuhusu nomino za kawaida na nomino za mguso ni mvurugo wa maelezo yanayotolewa. Sisi hatukuona tofauti kati ya nomino za mguso na nomino za kawaida. Zote zinarejelea dhana moja kwamba ni nomino zinazohusu vitu vya kawaida katika mazingira mbalimbali. Hata hivyo, tofauti za kimaelezo kati ya Walibora na Wang'endo (2004) na Vonyoli na wenzake (2018) zilitusaidia kushughulikia lengo letu la pili. Tulithibitisha kwamba, zipo tofauti za kimaelezo miongoni mwa waandishi wa Sarufi ya Kiswahili.

Wanafunzi walioshiriki katika utafiti huu walitupatia habari kwamba, baadhi yao hawajawahi hata kuiona Silabasi ya Kiswahili ya KIE (2002). 67 kati yao (asilimia 58%) walisema kwamba, hawajatangamana na silabasi ya Kiswahili kwa vile walimu wao hawajawafamisha.

Wanafunzi hawa hutegemea yaliyomo vitabuni au yale yanayowasilishwa na mwalimu wao. Tulipowahoji walimu nao walitufahamisha kwamba, ni kweli kwamba silabasi ya Kiswahili ipo ila baadhi yao hawajawafamisha wanafunzi wao. Licha ya kwamba silabasi ipo, baadhi ya walimu hawairejelei. Walimu 4 (asilimia 33) kati ya 12 walioshiriki katika uchunguzi huu walikiri kwamba, kwa muda mrefu wao hutengeneza matini yao kwa kutumia vitabu vya Sarufi ya Kiswahili na kulegea katika kuirejelea Silabasi ya Kiswahili. Tunapendekeza kwamba, kila mwalimu wa Sarufi ya Kiswahili na wanafunzi wawe na nakala za silabasi ya Kiswahili. Kwa kufanya hivyo, silabasi itawapa mwelekeo wa kitaaluma wakati wowote katika ufunzaji na ujifunzaji wa Sarufi ya Kiswahili.

Baada ya kubainisha tofauti hizo, tulichukua hatua ya kuchunguza mwelekeo uliotolewa na silabasi ya Kiswahili ya Taasisi ya Elimu ya Kenya (KIE, 2002). Silabasi hii inaelekeza kwamba, aina za nomino ni sita. Hizi ni: Nomino za kawaida/jumla, za pekee, dhahania, kitenzi jina, za jamii na nomino za wingi. Tunapendekeza kwamba, nomino za mguso zinazodokezwa na Walibora na Wang'endo (2004) zijumlishwe pamoja na nomino za kawaida ili tuwe na kundi moja tu la nomino za kawaida. Pia, tunapendekeza kwamba, walimu na wanafunzi wafuatilie yaliyomo kwenye Silabasi ya Kiswahili ya Taasisi ya Elimu ya Kenya (KIE, 2002) kila wakati. Silabasi hii ni chombo ambacho kinatoa mwelekeo uliofanyiwa utafiti na wataalamu wa Sarufi ya Kiswahili.

**Tofauti za Kimaelezo kuhusu Virai katika Sarufi ya Kiswahili**

Tulichambua matini kuhusu namna ambavyo dhana ya virai inavyofafanuliwa katika Sarufi ya Kiswahili na waandishi tofautitofauti. Tulifikia hili kwa kuchambua matini ya waandishi mbalimbali wa sarufi vya Kiswahili. Tulijikita katika lengo letu la pili katika utafiti huu lililoangazia kupambanua tofauti za kimaelezo kuhusu baadhi ya vipengele vya Sarufi ya Kiswahili. Kutokana na lengo hili, mojawapo ya tofauti za kimaelezo zilizogunduliwa na mtafiti ni kuhusu ufafanuzi wa dhana ya virai na aina zake kama inavyowasilishwa hapa chini. Tofauti hizi zinaonesha mitazamo kinzani baina ya waandishi tofautitofauti kama ifuatavyo:

Tulianza kwa kuchambua matini ya Vonyoli na wenzake (2018) katika kitabu chao cha *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Tatu*. Wanasema hivi:

Kirai ni neno au fungu la maneno ambalo ni sehemu ya sentensi na huwa ni kipashio cha kimuundo kisichokamilika kimaana. (Vonyoli na wenzake, 2018:119).

Kwa mujibu wa fasili hii, tunaona kwamba, kirai ni neno au fungu la maneno. Kirai kina muundo maalumu. Pia, kirai hakijitegemei kimaana. Kutokana na fasili hii, waandishi hawa wamevigawa virai katika makundi matano ambayo ni: Kirai nomino, kirai kitenzi, kirai kivumishi, kirai kielezi na kirai kihusishi. Ili kulinganisha maelezo haya na waandishi wengine, tulizamia kazi ya Ipara na Waititu (2011) katika kitabu chao cha *Ijarabu na Uikarabati.* Wao wanafafanua kirai hivi:

Kirai ni neno au kifungu cha maneno ambacho hutoa taarifa fulani. Virai hujengwa kwa aina moja tu ya neno pamoja na maneno yanayohusiana nayo, kama vile nomino na kivumishi au kitenzi na kielezi. (Ipara na Waititu, 2011: 73).

Kulingana na maelezo haya, kirai kinaweza kuwa neno moja au kifungu cha maneno. Kinatambulishwa kwa neno linalohusiana nacho. Kuna aina za virai kama vile kirai nomino, kirai kivumishi, kirai kitenzi na kirai kielezi.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.335

Aidha, tuliangazia mtazamo wa Ipara, Waititu na Okaalo (2015) katika kitabu chao cha *Kiswahili Fasaha Kidato cha Tatu* ili tubaini maoni yao kuhusu kirai. Nia yetu ilikuwa ni kulinganisha maelezo ya waandishi wengine kwa ajili ya kuthibitisha kuwepo kwa tofauti za kimaelezo. Tulipata ufafanuzi ufuatao kuhusu kirai:

Kirai ni neno au kifungu cha maneno ambacho hutoa taarifa fulani. Taarifa kamili hupatikana kutokana na kushirikiana kwake na maneno mengine katika sentensi. Virai hufanya kazi kutegemea aina za maneno yanayovijenga. (Ipara, Waititu na Okaalo, 2015: 166).

Tukiangazia kifungu hiki, tunaona kwamba kirai huwa na taarifa fulani. Taarifa hii hueleweka kutokana na kushirikiana kwake na maneno mengine katika sentensi. Mtafiti alidondoa mifano ya aina za virai kwa mujibu wa Ipara, Waititu na Okaalo (2015) ambayo walitambua kama virai vya nomino, virai vya vivumishi, virai elezi na virai vihusishi. Tulitafuta ufafanuzi zaidi kuhusu kirai kwa kurejelea maelezo ya Mogambi (2015) ambaye ameandika kitabu cha *Golden Tips.* Anadai:

Neno kirai limetokana na neno rai ambalo lina maana ya ombi au wazo. Kirai ni ombi dogo lisilo na maana kamilifu. Kirai ni kipashio cha kimuundo chenye zaidi ya neno moja lakini ambacho hakina kitenzi. (Mogambi, 2015:55).

Kulingana na dondoo hili, Mogambi (2015) anazua maelezo zaidi kuhusu kirai. Kwanza, anakiona kirai kama ombi au rai. Hapa, tathmini yetu ni kwamba, kirai si ombi au rai kwa sababu hakuna chochote kinachoombwa. Pili, kirai kina zaidi ya neno moja. Tatu, kirai hakina muundo wa kirai kitenzi. Kulingana na Mogambi (2015), kuna virai vya aina nyingi vikiwemo virai nomino, virai vielezi, virai vivumishi na virai viunganishi. Kutokana na maelezo haya, tulipata aina nyingine ya kirai ambayo ni kirai kiunganishi. Hapa hivi, tulibaini kuwa waandishi wengine hawajazungumzia kuwepo kwa kirai kiunganishi. Pia, Mogambi (2015) anadai kuwa, kuna aina nyingi ya virai. Hapa hivi, sisi tulielewa kwamba, virai havina idadi maalumu. Tuling'amua kuwa, mwandishi huyu ana mtazamo kwamba, virai ni vingi na havina idadi kamili kulingana na Sarufi ya Kiswahili. Tulizamia kudadisi mtazamo wa Wamitila (2004) katika *Chemchemi ya Kiswahili Kidato cha Tatu*. Maelezo yake ni kwamba:

Kirai ni tungo ambayo huundwa kwa maneno aghalabu mawili ambayo huwekwa kwa pamoja kuashiria kitu kimoja. Mpangilio au muundo wa kirai huzingatia uhusiano uliopo kati ya neno kuu na maneno mengine. (Wamitila, 2004: 213).

Katika kifungu hiki, kirai kinaundwa kwa maneno mawili kwa pamoja. Neno kuu ndilo hutambulisha aina ya kirai. Yeye anatambua kwamba kuna aina nne za virai katika Sarufi ya Kiswahili. Hizi ni: Virai nomino, virai vivumishi, virai vielezi na virai vihusishi. Katika orodha hii, hakuna muundo wa kirai kitenzi. Wataalamu Kiai na Maroko (2015) walidokeza kwamba, hakuna kitabu kimoja ambacho kina uwezo wa kukidhi mahitaji yote ya mwalimu au mwanafunzi. Kwa sababu hii, sisi pia hatukutosheka na maelezo ya Wamitila (2004). Kwa hivyo tulielekeza dira yetu katika kitabu cha *Longman* ambapo Omwaka na Gichuhi (2006) walisema yafuatayo kuhusiana na kirai:

Ni kipashio cha kimuundo chenye zaidi ya neno moja lakini ambacho hakina muundo wa kiima kiarifu. (Omwaka na Gichuhi, 2006: 22).

Kwa mujibu wa dondoo hili, kirai ni kifungu chenye zaidi ya neno moja. Pia, kirai hakina muundo wa kiima na kiarifu. Kulingana na wao, aina ya virai ni: Virai nomino, virai vitenzi, virai vivumishi, virai vielezi na virai viunganishi. Kutokana na uainishaji huu wa Omwaka na Gichuhi (2006), kuna muundo wa kirai kiunganishi kama alivyodai Mogambi (2015) katika kitabu chake cha *Golden Tips.* Kwa mujibu wa utafiti wetu, zipo tofauti baina ya waandishi. Tumeona kwamba Omwaka na Gichuhi (2006) na Mogambi (2015) wanatambua kuwepo kwa kirai kiunganishi. Mtazamo huu ni tofauti na anavyofasili Wamitila (2004), Ipara na Waititu (2011), Ipara, Waititu na Okaalo (2015) na Vonyoli na wenzake (2018). Kutokana na tofauti hizi, walimu wa Sarufi ya Kiswahili wana jukumu la kutathmini yaliyomo kwenye vitabu kabla ya kutekeleza ufundishaji.

Utafiti wetu ulithibitisha kwamba, asilimia 67% (N=77) ya wanafunzi walidai kwamba, tofauti za waandishi huwakanganya katika ujifunzaji wao. Tuliwasaili namna wanavyokabiliana na hali hii. Walitueleza kuwa, wakati mwingi wanajadiliana

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.335

katika vikundi, kusoma vitabu vingine na kuwauliza walimu wao ili wapate mwelekeo kuhusu baadhi ya maelezo ambayo wanafaa kutilia maanani miongoni mwa waandishi. Kwa kufanya hivyo, wanafunzi hawa hupata suluhu mathalan baadhi ya walimu huwapa fasili zao kwa mujibu wa tajiriba waliyo nayo katika uchambuzi wa vipengele vya Sarufi ya Kiswahili.

Maelezo kuhusu dhana ya virai yanaonesha kwamba, waandishi mbalimbali wa sarufi wana mitazamo kinzani kwa njia moja au nyingine kuhusu kipengele cha kirai. Kwanza kabisa, tulitambua kwamba, kuna ukinzani katika uainishaji wake. Kwa mujibu wa matokeo ya hapo juu, katika *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Tatu*, kuna aina tano za virai ambazo ni: Kirai nomino, kirai kitenzi, kirai kivumishi, kirai kielezi na kirai kihusishi. Uainishaji huu unaoana na ule unaopatikana katika *Ijaribu na Uikarabati* ambapo aina iliyodokezwa kuhusu virai ni kirai nomino, kirai kivumishi na kirai kitenzi. Hali hii ni tofauti katika *Kiswahili Fasaha* na *Golden Tips* ambapo kirai kitenzi hakitambuliwi kuwa mojawapo ya aina ya virai katika Sarufi ya Kiswahili. Nayo silabasi ya Taasisi ya Elimu ya Kenya (KIE, 2002) inaelekeza kuwa, mojawapo ya aina za virai ni virai vitenzi.

Mtazamo katika *Golden Tips* kuhusu kirai ni kwamba, ni kipashio chenye zaidi ya neno moja lakini ambacho hakina kitenzi. Kwa misingi hii, kulingana na mtazamo wa waandishi katika *Golden Tips* na *Kiswahili Fasaha Kidato cha 3*, hakuna aina ya kirai inayojulikana kama kirai kitenzi. Hii ni kinyume na hali ilivyo katika *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha 3* ambapo kuna kirai kitenzi. Dhana ya kirai kitenzi imeangaziwa na baadhi ya watafiti katika Sarufi ya Kiswahili kama vile msomi Habibu (2017). Habibu (2017) katika makala yake kuhusu muundo wa kirai kitenzi akilinganisha lugha ya Kiswahili na lugha ya Kisambaa alidokeza kwamba, kirai kitenzi kwa mujibu wa Massamba na wenzake (1999) ni kirai ambacho kimekitwa katika kitenzi au katika mahusiano ya kitenzi na neno au mafungu mengine ya maneno. Kulingana na dai hili, kirai kitenzi kipo katika Sarufi ya Kiswahili. Tukitilia mkazo ufafanuzi kama huu, waandishi ambao wana mtazamo kwamba hakuna muundo wa kirai kitenzi, wanakinzana na wenzao kama tulivyoona katika kitabu cha *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha 3* kwa mujibu wa maelezo haya:

Katika kirai kitenzi, kitenzi ndicho hutangulia. (Vonyoli na wenzake, 2018:119).

Kwa mujibu wa maelezo haya, waandishi wanatambua kwamba kuna kirai kitenzi. Hii inadhihirika kupitia kauli yao kwamba, **kitenzi ndicho hutangulia** katika muundo wa kirai kitenzi. Hapa wanazua mtazamo unaokinzana na ule wa Mogambi (2015) anaposema, kirai ni kipashio cha kimuundo chenye zaidi ya neno moja lakini ambacho hakina kitenzi. Ni dhahiri kwamba, mtazamo wa Vonyoli na wenzake (2018) ni kuwa, kuna muundo wa kirai kitenzi. Kwa upande mwingine, naye Mogambi (2015) anadai kuwa, hakuna muundo wa kirai kitenzi. Tofauti za aina hii ndizo mojawapo ya mitazamo kinzani miongoni mwa waandishi wa Sarufi ya Kiswahili. Tofauti hizi zinatatiza ufundishaji na ujifunzaji wa Sarufi ya Kiswahili. Hii ni kwa misingi kwamba, walimu na wanafunzi wanakanganywa hususan ni maelezo yepi ambayo yanaweza kuchukuliwa kuwa ndiyo faafu au ya kutegemewa. Kinachotokea hapa ni kuvurugwa kwa mawasiliano kati ya mwandishi na msomaji. Mawasiliano haya huvurugwa wakati ambapo waandishi wametumia lugha kuwasilisha jumbe ambazo zinakinzana kuhusu dhana moja. Kwa mfano, tumeona dhana ya kirai kitenzi ikielezwa kwa namna inayokinzana kwa mujibu wa waandishi tofauti. Hii imedhihirika katika matini ya waandishi hao. Matini hii katika Sarufi Amilifu ndiyo hubeba ujumbe wa mwandishi. Matini hii hutoa mawasiliano, mitazamo na mapendekezo ya mwandishi. Huu ndio utendaji wa lugha kama anavyodai Dik (1978). Utendaji huu huwasilisha ujumbe wa mwandishi kwa kupokelewa na msomaji anapopitia kazi yake. Hivyo basi, ujumbe huu unapokumbwa na mitazamo kinzani, huathiri upokeaji wa maarifa katika ufundishaji na ujifunzaji wa sarufi kama anavyodai Halliday (1994).

Maelezo yaliyotolewa na Omwaka na Gichuhi (2006) katika kitabu chao cha *Longman* yanazua utata zaidi unaodhihirisha mitazamo kinzani kati ya waandishi.Tuliegemea maneno “chenye zaidi ya neno moja” kuonesha utata unaoweza kusababisha mtazamo kinzani. Hii ni kwa sababu katika vitabu vingine kama vile *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Tatu*, kuna mifano ya virai vyenye neno moja tu! Kwa mfano, katika hiki cha *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Tatu*, mojawapo ya miundo katika kirai

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

nomino ni nomino moja ambapo kuna neno moja pekee.

Mifano iliyotolewa ni kama vile:

- Chakula kimepikwa.
- Mwalimu alisomesha jana.

(Vonyoli na wenzake, 2018: 119-120)

Kulingana na mifano hii, maneno yaliyopigiwa mstari ni kirai chenye neno moja. Katika sentensi ya (i), neno **chakula** ni kirai nomino na **kimepikwa** ni kirai kitenzi**;** vyote vikiwa na **neno moja pekee**. Aidha, **mwalimu** katika (ii) ni kirai nomino chenye neno moja. Hapa tunaona kwamba, maelezo haya yanakinzana na mtazamo wa Omwaka na Gichuhi (2006) wanapodai kuwa, kirai ni kipashio cha kimuundo **chenye zaidi ya neno moja**. Kando na Omwaka na Gichuhi (2006), Mogambi (2015) pia anadai kuwa kirai ni kipashio cha kimuundo chenye zaidi ya neno moja. Tazama maelezo yake:

Kirai ni kipashio cha kimuundo chenye zaidi ya neno moja lakini ambacho hakina kitenzi. (Mogambi, 2015: 55).

Kulingana na maelezo haya, mwandishi wa *Golden Tips* anaibua mambo mawili. Jambo la kwanza ni kwamba, kirai kina zaidi ya neno moja. Nalo la pili ni kuwa, hakuna muundo wa virai vitenzi. Tulichunguza na kutambua kwamba, licha ya kauli ya "**chenye zaidi ya neno moja**" katika *Golden Tips*, mifano iliyotolewa katika ukurasa huo huo inaonesha kirai chenye neno moja tu. Kwa mfano, kuna sentensi hizi:

- Mti umekauka.
- Kalamu imevunjika.

(Mogambi, 2015: 55-56).

Katika mifano hii, maneno yaliyopigiwa mstari katika (i) na (ii) ni virai nomino vyenye neno moja. Hapa tunaona kwamba, fasili iliyotolewa na mwandishi inakinzana na mifano ya mwandishi mwenyewe. Hii ni dhahiri shahiri kuwa, baadhi ya waandishi husababisha mitazamo kinzani katika matini yao wenyewe. Kwa mfano, matini katika fasili yanatofautiana na matini katika mifano inayotolewa kuhusu fasili hiyo. Kuwepo kwa matini kama hii katika Sarufi ya Kiswahili kunaathiri ufundishaji na ujifunzaji wake.

Tulikusudia kuthibitisha namna wanafunzi wanavyoathirika na hali kama hii. Uchunguzi wetu ulithibitisha kwamba, asilimia 62% (N=74) ya wanafunzi wanapokumbana na matini inayokinzana, wanakumbwa na changamoto. Walitueleza kuwa ili kukabiliana na changamoto hii, wao hurejelea vitabu vingine ili wapate maelezo kutoka kwa waandishi wengine. Kwa kufanya hivyo, wao hupata suluhu kwa baadhi ya changamoto zinazotokana na maelezo kinzani. Kwa misingi hii, hatua inayofaa kwa walimu na wanafunzi ni kurejelea vitabu anuwai kwa kusudi la kukadiria upungufu wa kimaelezo katika vitabu vingine.

Kimuhtasari, mtazamo wa Mogambi (2015) katika kitabu chake cha *Golden Tips* ni kwamba, aina za virai ni nyingi. Mtazamo huu unakinzana na maelezo ya akina Vonyoli na wenzake (2018) katika kitabu chao cha *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Tatu* ambapo wametambua aina tano maalumu za virai. Hali hii ni tofauti katika maelezo ya Waititu, Ipara na Okaalo (2004) katika kitabu chao cha *Kiswahili Fasaha Kidato cha Tatu* na Wamitila (2004) katika kitabu chake cha *Chemchemi ya Kiswahili Kidato cha Tatu* ambao wana aina nne maalumu za virai. Isitoshe, maelezo ya Omwaka na Gichuhi (2015) katika kitabu chao cha *Longman* ni kwamba, kuna aina tano kuu za virai. Idadi hii ni sawa na ile katika ufafanuzi wa Vonyoli na wenzake (2018) katika kitabu chao cha *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Tatu*. Tofauti iliyopo ni kwamba, Omwaka na Gichuhi (2015) wanatambua virai viunganishi ambavyo havitambuliwi na akina Vonyoli na wenzake (2018). Kwa kuzingatia haya, uchunguzi wetu umethibitisha kwamba kuna mitazamo inayokinzana miongoni mwa waandishi wa Sarufi ya Kiswahili. Tulirejelea silabasi ya Taasisi ya Elimu ya Kenya (KIE, 2002) kwa ajili ya kupata mwelekeo uliotolewa na wataalamu wa Sarufi ya Kiswahili. Silabasi hii inaelekeza hivi:

Aina za virai:

- Virai vihusishi
- Virai nomino
- Virai vivumishi
- Virai vielezi

(Silabasi ya KIE, 2002:42).

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.335

Kulingana na kifungu hiki, kuna aina nne za virai katika Sarufi ya Kiswahili. Tumeshuhudia kwamba baadhi ya waandishi wanatambua aina za virai kama vile virai vitenzi na virai viunganishi ambavyo havijatambuliwa na silabasi ya KIE (2002). Kwa vile silabasi hii ndiyo dira inayotoa mwelekeo sawa wa ufundishaji na ujifunzaji wa Sarufi ya Kiswahili, sisi tunawahimiza walimu na wanafunzi wazingatie yaliyomo kuhusu dhana ya virai.

**MUHTASARI**

Makala hii imeangazia tofauti za kimaelezo katika baadhi ya mada za Sarufi ya Kiswahili. Tumechambua matini ya waandishi wa Sarufi ya Kiswahili na kuonesha jinsi ambavyo wanakinzana katika ufafanuzi wa mada za Sarufi ya Kiswahili tulizorejelea. Uchanganuzi wetu uliongozwa na Nadharia ya Sarufi Amilifu inayosisitiza uzingatifu wa sarufi ya lugha katika utendakazi wake. Pia, tulitumia nadharia ya Ujifunzaji Kitajiriba. Sehemu kubwa ya data tuliyokusanya ilitokana na uchanganuzi wa yaliyomo ambapo tulichambua matini katika kazi za waandishi wa Sarufi ya Kiswahili kama ilivyo katika vitabu vya kiada na vya ziada vinavyotumika katika shule za upili nchini Kenya. Mbinu nyingine tulizotumia ni hojaji na mahojiano. Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kwamba, baadhi waandishi wa Sarufi ya Kiswahili wanatofautiana kimaelezo, kimfano au kifasili katika baadhi ya mada za Sarufi ya Kiswahili. Tumependekeza kwamba Taasisi ya Ukuzaji wa Mitalaa ya Kenya itilie mkazo tofauti za kimaelezo baina ya waandishi wa Sarufi ya Kiswahili kwa ajili ya kutoa matoleo mapya yaliyofanyiwa marekebisho.

**MAREJELEO**

Abai, R. A., & Nyandiba, C. (2019). Athari za Uandishi na Uchapishaji wa Vitabu vya Kiada katika Ufundishaji wa Kiswahili nchini Kenya. Katika Kobia, J. M., Kandagor, M., Mwita, L. C., Mataira, J. N. na Simwa, S. P. (Wahariri) (2019). *Uwezeshwaji wa kiswahili kama wenzo wa maarifa*. Eldoret: Moi University Press.

Bruno, E. (2020). *A grammar of paraquayan guarani: Phonology and orthography: the sound system and its written representation*. UCL Press. Downloaded from https://www.jstor.org/ /stable/j.ctv13xpscn.8.

Dik, C. S. (1978). *The Theory of Functional Grammar:* Part 1: The Structure of the Clause. Dordrecht: Foris.

Habibu, N. (2017). Muundo wa kirai kitenzi katika lugha ya Kisambaa. Juzuu ya 21. Kutoka nasra.habibu@out.ac.tz.

Halliday, M. A. K. (1994). Functional Grammar. Birmingham: University of Birmingham Press.

Ipara, I. & Waititu, F. (2011). Ijaribu na Uikarabati: Marudio ya KCSE Kiswahili. Nairobi: Oxford University Press, East Africa Ltd.

Kiai, A.W. & Maroko, G. M. (2013). *Textbook Selection Experiences among Secondary School Teachers of English in Kenya*. International Journal of Education and Research: Vol. 1 No. 12.

Kolb, D. A. (1984). *Experiential Learning Theory. A Dynamic, Holistic Approach to Management Learning, Education and Development. Downloaded* at: https://www.researchgate.net/publication/267974468

Kolb, D. A. & Kolb, A, Y. (2011). *Experiential Learning Theory: A Dynamic, Holistic Approach to Management Learning, Education and Development. Inapatikana*: https://www.researchgate.net/publication/267974468.

Landrum, R. E., Gurung, R.A.R & Spann, N. (2012). *Assessments of Textbook Usage and the Relationship to Student Course Performance*. Boise: Taylor and Francis Group, LLC.

Leigh, L. (2007). *The power of prepositions*. Cairo: Criminal Brief Press.

Massamba, D. T., Kihore, M.Y. & Hokororo, J. I. (1999). *Sarufi miundo ya Kiswahili sanifu* (SAMIKISA). Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.335

Mogambi, H. (2015). *Golden Tips: Kiswahili Kwa Shule za Upili*. Nairobi: Moran (E.A.) Publishers Limited.

Mumbo, C. K. & Ngamia, F. O. (2003). *Johari ya Kiswahili: Kidato cha Pili*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Navaz, A. M. N. & Sama, F. R. F. (2018). *Teaching grammar in the English language classroom*: Perception and Practices of students and teachers in the Ampara District. Sirlanka: South Eastern University of Sirlanka Press.

O'Neill, R. (1982). *Why use textbooks?* ELT Journal, Vol 36, Pages 104-111.

O'Grady, W., Dobrovolsky, M., & Katamba, F. (1996). *Contemporary Linguistics: An introduction.* Harlow Essex, Longmna Publishers.

Omwaka, H. & Gichuhi, N. (2006). *Longoman: Marudio ya KCSE*. Longman Kenya Ltd.

Olodo, R. & Njogu, K. (2005). *Tanzu za Lugha: Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Nne*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Richards, J.C. (2001). *The Role of Textbooks in a Language Programme*. Cambridge: Seameo Relc Publication.

Timammy, R. & Oduor, A. J. O. (2016). *Treatment of Kiswahili in Kenya's Education System*. Nairobi: University of Nairobi Journal of Language and Linguistics.

Tomlinson, B. (1998). *Materials Development in Language Teaching*. United Kingdom: Cambridge University Press.

Wamitila, K. W. (2004). *Chemchemi za Kiswahili: Kidato cha Tatu*. Nairobi: Longhorn Publishers (Kenya) Ltd.

Wamitila, K. W. (2015). *Chemchemi za Kiswahili: Kidato cha Nne*. Nairobi: Longhorn Publishers (Kenya) Ltd.

Wamitila, K. W. & Waihiga, G. (2010). *Chemchemi za Kiswahili: Kidato cha Pili*. Nairobi: Longhorn Publishers (Kenya) Ltd.

Walibora, K. & Wang'endo, F. (2004). *Uhondo wa Kiswahili: Kwa Shule za Upili Kitabu cha Mwanafunzi Kidato 1*. Nairobi. Moran (E. A.) Publishers Limited.

Waititu, F., Ipara, I. & Okaalo, B. (2015). *Kiswahili Fasaha, Kidato cha Tatu*. Nairobi: Oxford University Press.

Waititu, F., Ipara, I., Okaalo, B. & Vuzo, A. (2004). *Kiswahili Fasaha, Kidato cha Pili*. Nairobi: Oxford University Press.

Waititu, F., Ipara, I., Okaalo, B. & Vuzo, A. (2004). *Kiswahili Fasaha, Kidato cha Tatu*. Nairobi: Oxford University Press.

Waititu, F., Ipara, I. & Okaalo, B. (2003). *Kiswahili Fasaha, Kidato cha Kwanza*. Nairobi: Oxford University Press, East Africa Ltd.

Wong, V. & Bar-Yam, Y. (2017). How do people differ? A Social Media Approach. Cambridge: 210 Broadway Publication.

Vonyoli, A. J., Watuha, A. I., Mutekwa, F. O., Makombo, H. S., Maina, K. D. & Waweru, M. (2014). *Kiswahili Kitukuzwe: Kwa Kidato cha Kwanza, Kitabu cha Mwanafunzi* (Toleo la Tano). Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Vonyoli, A. J., Watuha, A. I., Mutekwa, F. O., Makombo, H. S., Maina, K. D. & Waweru, M. (2014). *Kiswahili Kitukuzwe: Kwa Kidato cha Pili, Kitabu cha Mwanafunzi* (Toleo la Tano). Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Vonyoli, A. J., Watuha, A. I., Mutekwa, F. O., Makombo, H. S., Maina, K. D. & Waweru, M. (2014). *Kiswahili Kitukuzwe: Kwa Kidato cha Tatu, Kitabu cha Mwanafunzi* (Toleo la Tano). Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Vonyoli, A. J., Watuha, A. I., Mutekwa, F. O., Makombo, H. S., Maina, K. D. & Waweru, M. (2014). *Kiswahili Kitukuzwe: Kwa Kidato cha Nne, Kitabu cha Mwanafunzi* (Toleo la Tano). Nairobi: Kenya Literature Bureau.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.